epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Mei 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581685
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22
**MAMA MBAPPÉ AFICHUA MWANAWE ANATUA MADRID**

# WHO: UKIMWI haujapungua



• **Magonjwa** ya zinaa, homa ya ini balaa tupu... *Endelea ukurasa*



**Milioni moja waambukizwa kila mwaka**

**Yanaua watu milioni 2.5 kila mwaka**





**Rais wa Wauguzi aanika hali halisi, staili yao ya kupambana**



## Aliyesotea haki kazini miaka 32 kulipwa mil. 207/-

UKURASA 7

UKURASA WA 5
**SAMIA KUWAKUSANYA DAR JK, WASTAAFU WENZAKE WA AFRIKA**



UKURASA WA 16
**MAOFISA TASAF 'FEKI' WADAIWA KUTOZA FEDHA KWA WANANCHI**

UKURASA WA 19
**WAKENYA WALIA NA RAIS WAO KUKODI NDEGE KWA BIL. 3.9/- KUZURU USA**



## Sheria mpya ya Ndoa yaja

• **Malasusa:** Kuna shida kubwa uandikaji wosia...
*Endelea ukurasa wa 7&8*

**MICHEZO** **FEI TOTO: TUNAITAKA LIGI YA MABINGWA** UK.24 **KATUNI** UK.6

## LHRC yamvaa mwandishi madai ya udhalilishaji dhidi ya wanawake

**Na Jenifer Gilla**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimekemea tabia ya mwandishi na mchambuzi wa habari za michezo, Oscar Oscar, kutengeneza na kusambaza maudhui yenye mlengo wa kumdhalilisha mwanamke kwenye mitandao ya kijamii.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, ilisema mwandishi huyo amekuwa na kawaida ya kutengeneza vibonzo vyenye maudhui hayo na kuyasambaza kwenye ukurasa wake wa X na Instagram kinyume cha Sheria ya Mitandao.

Kupitia taarifa hiyo, Dk. Henga alisema mwandishi huyo amejizolea umaarufu kwa maudhui ya aina hiyo na yamekuwa yanawafikia watu wengi kutokana na umaarufu wake.

"Kituo kinatoa onyo kwa ndugu Oscar Oscar na kumtaka kuacha mara moja kuweka maudhui ya udhalilishaji dhidi ya wanawake kwenye mitandao ya kijamii, vinginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake," ilisema taarifa hiyo.

Dk. Henga alimwekeleza mwandishi huyo kuzingatia Ibara ya 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoelekeza kulinda heshima, kuthamini utu wa mtu na kupinga ubaguzi wa aina yoyote.

Alisema kitendo anachokifanya Oscar ni kinyume cha Mkataba wa Kimataifa wa Kupinga Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa 1979 unaosisitiza ubaguzi dhidi ya wanawake unakiuka kanuni za usawa wa haki na heshima kwa hadhi ya binadamu.

Maudhui hayo, alisema hayadhalilishi tu wanawake bali huwafanya waonekane kama chombo cha starehe, dhihaka na kuwaonyesha kama binadamu wasio na mchango katika jamii katika nchi hiyo iliyopiga hatua kubwa kulinda haki za wanawake.

Alitoa rai kwa watumiaji wote wa mitandao ya kijamii kuitumia kama chanzo cha kuelimisha jamii na sio kwa lengo la kupotosha au kudhalilisha jamii hasa wanawake.

## TANGAZO LA KIFO



**DKT. SUZANE HENRY MPONZI**
**(FEB. 1969 – DIS. 2023)**

Ndugu Inj. Naseeb Mohamed Mpembule wa Upanga Dsm, Anasikitika Kutangaza Kifo Cha Mke Wake Mpendwa **Dkt. SUZANE HENRY MPONZI**, Kilichotokea Jumamosi **Tarehe 23/12/2023**, Katika Hospitali ya Regency Jijini Dsm, Baada ya Kuugua Kwa Muda Mfupi. Mazishi Yalifanyika Jumanne **Tarehe 26/12/2023**, Nyumbani Kwake Kibaoni-Ifakara, Mkoani Morogoro.

**Habari Ziwafike:**

- Mtoto wa Marehemu, Munilisa Mpembule Wa Upanga (Dsm)
- Familia Ya Mzee Mponzi Na Lyuvale Popote Pale Waliko
- Familia Ya Mzee Mpembule Na Lihimba Popote Pale Waliko
- Kaka Zake, Dada Zake Na Wadogo Zake Popote Pale Waliko
- Uongozi, Madaktari, Wauguzi Na Wafanyakazi Wote Wa Hospitali Ya Mnazi Mmoja (Dsm)
- Uongozi wa Masjid Ma'amur (Dsm) Na Quba (Ifakara)
- Ndugu, Jamaa Na Marafiki Popote Pale Waliko.

*'INNAA LILLAAHI WA INNAA ILAYH RAAJIUUN'*

# WHO: UKIMWI haujapungua

**Na Romana Mallya**

RIPOTI mpya ya Shirika la Afya Duniani (WHO) inaonesha bado kuna changamoto za Virusi vya UKIMWI (VVU) na homa ya ini duniani.

Vilevile, zaidi ya watu milioni moja wa umri wa kuanzia miaka 15 hadi 49 huambukizwa magonjwa ya zinaa ikiwamo kaswende na kisonono kwa mwaka.

Katika ripoti hiyo iliyotolewa juzi, inaelezwa kwamba maambukizi mengi yanatokea barani Afrika na Amerika, huku magonjwa ya zinaa yakiongezeka katika maeneo mengi.

Mwaka 2022, nchi wanachama wa WHO ziliweka lengo kubwa la kupunguza idadi ya kila mwaka ya maambukizi ya kaswende kwa watu wazima mara 10 ifikapo 2030 kutoka watu milioni 7.1 hadi milioni 0.71.

Hata hivyo, maambukizi mapya ya kaswende miongoni mwa watu wazima wenye umri wa miaka 15 hadi 49 yaliongezeka kwa zaidi ya milioni moja mwaka 2022 na kufikia milioni nane mwaka jana, ikiwa ni ongezeko la juu zaidi lililotokea katika kanda za Amerika na Afrika.

### VVU/UKIMWI

Ripoti ya WHO imeonesha VVU, homa ya ini na magonjwa ya zinaa husababisha vifo milioni 2.5 kila mwaka, takwimu mpya zikionesha watu zaidi walifariki dunia kutokana na sababu zinazohusiana na homa ya ini, milioni 1.3 mnamo 2022 kulinganishwa na milioni 1.1 mwaka 2019.

Inaelezwa katika ripoti hiyo kuwa kwa siku kuna maambukizi mapya kwa watu milioni moja, wengi wao wakipata maambukizi kwa njia ya zinaa.

"Ongezeko la kesi mpya za maambukizi ya magonjwa ya zinaa linazidi kuripotiwa katika nchi nyingi wanachama wa WHO," ripoti inabainisha.

Inaelezwa katika ripoti hiyo kuwa maambukizi ya VVU na homa ya ini pia hayapungui kama ilivyotarajiwa kuelekea ukomo wa upimaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, mwaka 2030.

Zaidi ya asilimia 75 ya watu wanaoishi na HIV wanapata huduma ya dawa za kupunguza makali ya VVU wakati asilimia 93 ya walio kwenye tiba, wana kinga iliyo chini ambayo haitaki ARV, ripoti inaeleza.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kupungua kwa vifo vinavyotokana na homa ya ini aina ya C kutoka 290,000 mwaka 2019 hadi kufikia vifo 240,000 mwaka 2022 kunaashiria kuongezeka upatikanaji wa matibabu yake.

Mwaka 2023, Misri ilifikia kiwango cha juu kabisa kuondoa homa ya ini aina ya C ikionyesha mafanikio yanawezekana kwa nchi yenye kipato cha chini na wastani, ripoti inaeleza.

WHO inasema katika ripoti yake kuwa nchi nyingi tayari zimeendeleza mikakati ya kiafya ya kuzuia maambukizi ya VVU na kaswende kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

"Kuongezeka kwa matukio ya kaswende kunazua wasiwasi mkubwa," Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Ghebreyesus amenukuliwa katika ripoti hiyo.

"Kwa bahati nzuri, kumekuwa na maendeleo muhimu katika nyanja zingine kadhaa ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya upatikanaji bidhaa muhimu za afya, hasa uchunguzi na matibabu," anasema.

### HALI ILIVYO NCHINI

Waziri wa Afya nchini, Ummy Mwalimu, wiki iliyopita alipowasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi yake kwa mwaka wa fedha 2024/25, alitaja malengo mbalimbali ya serikali katika kukabiliana na magonjwa, yakiwamo ya zinaa yanayomulikwa katika ripoti tajwa ya WHO.

Alisema malengo hayo ni pamoja na kupunguza maambukizi ya kaswende kwa asilimia 90, kupunguza maambukizi ya Kisonono kwa asilimia 90 na kupunguza maambukizi ya kaswende ya kuzaliwa kwa watoto wachanga kufikia visa 50 au chini kwa kila watoto 100,000 waliozaliwa hai.

Ummy alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024, wajawazito 1,761,156 sawa na asilimia 88.6 walipima maambukizi ya kaswende kulinganishwa na wajawazito 1,663,808 sawa na asilimia 98.8 waliopima maambukizi ya kaswende kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

Alisema kuwa katika kipindi hicho, asilimia 0.65 ya wajawazito walikutwa na maambukizi ya kaswende na kupatiwa matibabu.

Alirejea Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI (Tanzania HIV Impact Survey - THIS) wa mwaka 2022/23, uliobaini kiwango cha ushamiri wa VVU kimepungua kutoka asilimia 4.7 mwaka 2016/2017 hadi kufikia asilimia 4.4 mwaka 2022/23 kwa watu wenye umri kuanzia miaka 15.

### CHAMA CHA WAUGUZI

Rais wa Chama cha Wauguzi Tanzania, Alexander Baluhya, alipotafutwa na mwandishi wa habari hizi jana kuzungumzia ripoti mpya ya WHO, alisema kwa Tanzania maambukizi ya magonjwa hayo yameshuka kutokana na kutolewa elimu kwa umma.

"Kisonono na kaswende ni magonjwa ambayo yalikuwa na unyanyapaa na kutengwa. Baada ya elimu na ushirikishwaji wa karibu, watu wengi hufika sehemu za kutolea huduma na kufanya uchunguzi wa awali na kupata tiba.

"Zamani zilikuwa ni kliniki za UKIMWI, ikawa ni sehemu za huduma zozote kwa kuwa watu walihofu kwenda kufanya uchunguzi, ulikuwa ukionekana unakwenda sehemu fulani wanasema 'haa tayari ana magonjwa ya zinaa'. Hili limeondolewa na kuwa huduma mbadala kama mtu mwenye malaria," alisema.

### UAMBUKIZAJI

Baadhi ya Watanzania kupitia mitandao ya kijamii, baada ya kusoma ripoti mpya ya WHO, wamenyoosha kidole kwa wanaoendekeza ngono zembe kuwa wanaweza kuangukia katika magonjwa hayo. Baadhi yao walitaka kujua uambukizwaji wa kaswende kwa mwanamke na mwanamume.

Katika hilo la uambukizwaji wa ugonjwa huo, Daktari wa Binadamu, Albert Robert alisema, "Kaswende au syphilis - (kwa Kiingereza), ni ugonjwa wa zinaa unaosababishwa na bakteria aitwaye Treponema Pallidum.

"Ugonjwa huu unaweza kuwa na madhara makubwa kwa wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 15 hadi 49, hasa katika masuala ya uzazi."

Dk. Robert alitaja madhara kwa wanawake ni mimba kutunga nje ya mfuko wa uzazi ambapo kaswende inaweza kusababisha maambukizi katika mirija ya uzazi, hivyo kuongeza hatari ya mimba kutunga nje ya mfuko wa uzazi.

Alitaja madhara mengine ni mwanamke kuzaa watoto si riziki (waliofia tumboni) na kujifungua kabla ya muda. Kitaalamu ujauzito uliokamilika ni wa kuanzia wiki 37 hadi 38.

Daktari huyo alisema ugonjwa huo usipotibika unaweza kusababisha mimba kuharibika, kuzaa mtoto kabla ya muda wake au kuzaa mtoto si riziki na kuna uwezekano wa kuzaa mtoto mwenye maambukizi ya kaswende.

Madhara mengine alisema ni ugumba (infertility) ambapo mwanamke anapokuwa na maambukizi ya muda mrefu yanaweza kuharibu mfumo wa uzazi, ikiwa ni pamoja na mirija ya uzazi na mfuko wa uzazi, hivyo kusababisha ugumba.

Kwa upande wa wanaume, Dk. Robert alitaja madhara ni pamoja na kupungua kwa ubora wa mbegu za kiume.

Alitaja madhara mengine ni kuvimba kwa korodani kutokana na maambukizi ya muda mrefu, kupata maumivu na kupunguza uzalishaji mbegu.

"Madhara mengine ni kupungua kwa uwezo wa kutungisha mimba. Madhara ya muda mrefu ya kaswende yanaweza kuathiri uwezo wa mwanamume kutungisha mimba," alisema.

Dk. Robert alitaja madhara ya pamoja kwa mwanamume na mwanamke ni kuongeza hatari ya maambukizi mengine ya zinaa ikiwa ni pamoja na HIV.

"Pia kuathiri mfumo wa neva na moyo ambapo katika hatua za mwisho za kaswende, ugonjwa unaweza kuathiri mfumo wa maeneo hayo na kusababisha matatizo ya ulemavu wa kudumu au kifo," alisema.

HABARI KITAIFA

# Viwanda kuongeza thamani kuchochea uchumi kujengwa

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI imetenga eneo la Buzwagi mkoani Shinyanga, kuwa Eneo Maalum la Uwekezaji (Buzwagi Economic Process Zone), kwa ajili ya kujenga viwanda vya kuongeza thamani madini na kuchochea shughuli za kiuchumi.

Lengo la viwanda hivyo ni kupunguza ununuzi wa bidhaa zinazohitajika kwenye migodi nje ya nchi wenye thamani ya Sh. trilioni 3.1

Waziri wa Madini, Athony Mavunde, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa jukwaa la tatu la utekelezaji wa ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini.

Alisema eneo la Kahama zimetengwa ekari 1,331 zinazosubiri wawekezaji kwa ajili ya kuanzisha viwanda mbalimbali na kwamba viwanda vinane vikubwa duniani vikiwa tayari vimeonyesha nia ya kufanya uwekezaji katika eneo hilo.

Alisema moja ya hatua ambazo serikali imeamua kuichukua ni kuboresha ushirikishwaji wa wazawa katika uwekezaji huo.

"Najua tozo ziko na zina utaratibu wake lakini eneo hili sasa kama serikali tunalolipa kipaumbele kikubwa sana ni eneo la 'local content' (ushirikishwaji wazawa).

"Na nitawaambia kwa nini. Ununuzi uliofanywa katika sekta ya madini kwa mwaka wa fedha uliopita, ni zaidi Sh. trilioni 3.1 yaani hii migodi yote iliyoko hapa nchini, imefanya manunuzi ya Sh.trilioni 3.1.

"Fedha hii ikibaki Tanzania inatugusa sisi, inabadilisha uchumi wetu, uchumi wa kaya, uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Ili tuwaone Watanzania wengi zaidi wananufaika na sekta hii ya madini, nitoe rai kwa ndugu zangu kuchangamkia fursa hii. Natamani kuziona Sh. trilioni 3.1 zinabaki nchini," alisema.

"Na ndio maana nimewaelekeza Tume ya Madini katika procurement plan (mpango wa ununuzi) waniletee orodha ya bidhaa ambazo zinaagizwa kutoka nje ya nchi ili sisi tuwatafute hao wazalishaji wa nje ya nchi waje wawekeze Tanzania, Watanzania wanufaike na fursa hiyo. Vilevile ili kuweza kukuza uchumi wetu wa Tanzania," aliongeza.

Kwa mujibu wa Waziri Mavunde, lengo la wizara yake ni kuifanya Tanzania iwe kitovu cha utoaji wa huduma za sekta ya madini Afrika Mashariki na Kati na Afrika ya Kati.

"Tunataka watu wote wapate bidhaa kutokea Tanzania na jambo hili ndugu zangu Watanzania linawezekana. Leo pale Kahama tuna East African Conveyers Limited, ambao wanazalisha 'conveyer belts', wanasambaza katika migodi yote ya Barick, North Mara, Bulyankulu na mpaka nchini Congo DRC. Na hii ni kampuni ambayo Watanzania wameingia ubia na ni vijana wa Kitanzania.

Pia alisema kampuni ya Max Steel inayozalisha vifaa vya kushikilia miamba (wiremesh na bolts) hivi sasa inakamilisha ujenzi wa kiwanda hicho na Watanzania watapata huduma ndani ya nchi badala ya kuagiza nje ya nchi.

Pia alisema kampuni ya kimataifa ya Rock Solution ambayo inatengeneza vifaa vinavyotumika kutunza sampuli za miamba, iko asilimia 90 kukamilisha mradi huo na kwamba muda si mrefu Watanzania wataanza kuona bidhaa nyingi zinazalishwa nchini Tanzania.

"Maono ya 2030 maana yake ni kwamba ikifika mwaka 2030, tutakuwa tumefika asilimia 30 ya eneo la nchi yetu ya Tanzania kufanyiwa utafiti wa kina. Leo tuna uwezo wa kujua madini yako wapi lakini hatujui kwa kiwango gani. Ukijua ni kwa kiwango gani ni rahisi kupanga mipango yetu.

**UTAFITI**

Katika jukwaa hilo linaloongozwa na kaulimbiu 'Uwekezaji wa Viwanda vya Uzalishaji wa Bidhaa za Migodini kwa Maendeleo Endelevu', Waziri Mavunde alisema eneo la Tanzania lililofanyiwa utafiti mpaka sasa ni asilimia 16 tu, lakini nchi imeendelea kupata manufaa makubwa.

Katika eneo la 'local content' kwenye sekta ya madini, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2023, ajira zilizozalishwa ni 18,853, sawa na ongezeko la ajira 2,391 ambayo ni asilimia 14.5

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Msafiri Mbibo, alisema majukumu ya ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini, ni kuhakikisha kipaumbele kinatolewa kwa huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini na Watanzania katika sekta ya madini.

Mbibo pia alisema kupokea mipango ya ushirikishwaji wa Watanzania (local content) na kuichambua kwa ajili ya kuidhinishwa.

Mengine ni kusimamia na kuidhinisha utolewaji wa mikataba ya manunuzi ya bidhaa na huduma kwa wamiliki wa leseni za madini na watoa huduma katika sekta ya madini.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Cynthia Mwilolezi.***


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende "pay via mobile". Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-6



Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Wafanyabiashara wabanwa kodi

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesisitiza kuwa ni lazima wafanyabiashara walipe kodi ili kutekeleza miradi ya maendeleo huku ikiwahakikishia kuwa imejizatiti kulinda maslahi yao katika Kituo cha Biashara cha Afrika Mashariki.

Katika michango yao jana na juzi kwenye makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, wabunge waliishauri serikali kulinda maslahi ya wafanyabiashara wazawa katika kituo hicho kinachojengwa Ubungo, Dar es Salaam.

Wabunge pia waliikumbusha serikali maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuwa wafanyabiashara wasifanyiwe kutathmini ya madeni ya kuanzia miaka mitatu iliyopita. Akijibu hoja hizo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali itawafanyia tathmini ya madeni yaliyozidi miaka mitatu wafanyabiashara wakubwa kwa sababu wamebeba kodi nyingi za wafanyabiashara wadogo.

Alisema wafanyabiashara hao wamepewa dhamana ya kukusanya kodi za wengine na kuzifikisha serikalini lakini wanazitumia kujitajirisha, hivyo serikali lazima itawafanyia tathmini hata kama imepita miaka 10.

"Hawezi kugeuza hiyo ni fedha yake. Tutaenda naye sambamba hata kama imepita miaka ya kutosha ni lazima ailipe," alisema Dk. Nchemba.

Alisema katika kundi hilo, kuna wazabuni waliokata rufani katika Bodi ya Wazabuni wakidaiwa Sh. trilioni 6.5 za kodi na uamuzi wa Sh. trilioni 3.2 umefanyika na kuna walioambiwa walipe. Pia alisema kuna kesi za madai ya kodi ya Sh. trilioni mbili ambazo wafanyabiashara wamekata rufani katika Baraza la Rufani la Kodi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema ili kuhakikisha inalinda wafanyabiashara wazawa katika Kituo cha Biashara cha Afrika Mashariki. Serikali imeweka utaratibu kuwa asilimia 95 ya vibanda vya biashara vitavimilikiwa na Watanzania.

Alisema eneo hilo lina vibanda 1,860 na kati ya hivyo, 985 vimeshachukuliwa na wafanyabiashara huku wageni wakiwa 15 tu. Pia alisema kutakuwa na maghala ya kuhifadhia mizigo na forodha.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema katika juhudi za kulinda wazalishaji wa ndani wa mafuta, wizara hiyo imepeleka mapendekezo Wizara ya Fedha ya kuanza utaratibu wa kuingiza mafuta ya nje pale ya ndani yatakapokwisha.

Alisema pia serikali itaongeza kodi kwenye mafuta ghafi na mafuta masafi kwenye mafuta ya alizeti yanayotoka nje ili kulinda masoko ya ndani.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema serikali ina mpango wa kuweka viwanda katika mtaa mmoja kila wilaya ili kuchakata malighafi zinazozalishwa kwa wingi katika wilaya husika.

Alisema serikali pia inaendelea kuwalinda wawekezaji wa ndani na wa nje huku wakihakikisha wafanyakazi katika viwanda hivyo wanapata stahiki zao muhimu ikiwamo kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Dk. Kijaji alisema katika ukaguzi waliofanya kwenye viwanda 22 nchini, walikuta changamoto ya maslahi ya wafanyakazi kwenye kiwanda kimoja tu kilichoko wilaya ya Temeke na tayari ameshaikabidhi kesi hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).

Aliwakumbusha wafanyabiashara wakubwa na wadogo nchini kuwa waadilifu na kufuata sheria ili waepuke kujiingiza kwenye matatizo, hivyo kushindwa kufikia dhamira waliyoiwekea katika biashara zao.




Mkurugenzi Mkuu wa Ecobank Tanzania, Dk. Charles Asiedu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa uzinduzi wa huduma ya mikopo ya riba ya asilimia 12 kwa watumishi wa umma, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mkuu wa kitengo cha Wateja Binafsi, Ruth Mwaiselage na Meneja Mwandamizi wa Bidhaa za Walaji, Innocent Urio. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ecobank yaanzisha huduma mikopo kwa watumishi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Ecoback Tanzania imeanzisha huduma ya utoaji mikopo kwa watumishi wa umma kwa riba ya asilimia 12, mtumishi akitakiwa kulipa katika kipindi kisichozidi miaka saba.

Huduma hiyo inalenga watumishi wote wa umma ili kufikia malengo yao ambayo wanataka kuyakamilisha kwa haraka na kwa njia rahisi.

Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Dk. Charles Asiedu, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumzia fursa hii ya mikopo kwa watumishi wa umma.

"Ni wakati sasa wa benki hii kuwafikia watumishi wa umma katika sekta mbalimbali na kuwapatia huduma muhimu ya mikopo ili kuinua vipato na maisha yao kwa ujumla," alisema Dk. Asiedu.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Ruth Mwaiselage, alisema benki hiyo itatoa mikopo ya hadi Sh. milioni 125 kwa taasisi mbalimbali za serikali kwa riba ya asilimia 12.

Alisema mtumishi wa umma anaweza kulipa katika e za fedha, Ecobank itanunua mikopo yao ili kuwapa nafasi ya kuongeza zaidi ili kuyafikia malengo yao," alisema.

Ruth alisema akaunti ya watumishi wa umma ni ya bure na haina makato ya mwezi na kufafanua kuwa mikopo hiyo ina bima ya maisha kumlinda mkopaji endapo kitatokea kifo, ulemavu wa kudumu au kupunguzwa kazi.

Alisema ili mtumishi kupata mkopo, anatakiwa kufungua akaunti ya Ecobank kupitia matawi yaliyoko Dar es Salaam, Arusha na Mwanza.

**Ni wakati sasa wa benki hii kuwafikia watumishi wa umma katika sekta mbalimbali na kuwapatia huduma muhimu ya mikopo ili kuinua vipato na maisha yao kwa ujumla.**

# Congo kununua tani 500,000 mahindi Tanzania

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKALA wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), imetia saini mkataba wa mauziano ya mahindi tani 500,000 na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa ajili ya kuwasaidia upatikanaji wa chakula kwa nchi hiyo.

Mkataba huo wameingia na kampuni ya Quincy iliyopo Jimbo la Katanga, nchini DRC, lengo ikiwa ni kuwasaidia upatikanaji wa chakula.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweri, alisema katika mkataba huo DRC awamu ya kwanza wataondoka na tani 200,000 na awamu nyingine watamalizia tani 300,000.

Mweri alisema wameanza ushirikiano huo wa kufanya biashara ya mazao, kama moja ya mkakati waliouweka kwa ajili ya kuwa kitovu cha uzalishaji wa chakula nchini na barani Afrika kwa ujumla.

"Tumeanza kuwauzia tani hizo za mahindi, tuna akiba ya chakula katika maghala yetu na tayari tumefungua vituo 14 vya kukusanyia mazao hapa nchini," alisema Mweri.

Alifafanua kuwa serikali imetenga Sh. bilioni 300 kwa ajili ya uwekezaji wa kununua mazao ya chakula tani 300,000, msimu unapoanza NFRA itaanza ukusanyaji wa mazao ya chakula.

Amewashukuru DRC kwa kusaini mkataba huo, pia kuna nchi nyingine ambazo zinanunua mahindi kutoka hapa nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa NFRA, Dk. Andrew Komba, alisema msimu unaoanza Julai mosi, wataanza ukusanyaji wa mazao ya chakula kama mahindi, mpunga na mazao mengine.

Alisema wamejipanga kuhakikisha taifa linakuwa na akiba ya kutosha ya chakula na kuongeza kuwa wananchi wasiwe na wasiwasi wowote kuhusu chakula.

Alisema lengo lao kama serikali ni kuhakikisha chakula kinakuwapo cha kutosha, ili wananchi wasiteseke kukipata kinapohitajika.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Quincy kutoka Congo, Yuma Gerard Jesse, aliishukuru serikali kutokana na kukubali kutia saini mkataba wa kuuziana mazao ya chakula.

Alisema wanaipongeza Tanzania, hususani Wizara ya Kilimo kutokana na kuendesha kilimo kwa ufasaha kwa wakulima na kuuza mazao mpaka nje ya nchi.

Gavana wa Jimbo la Katanga, Jacques Katwe, alisema amekuja Tanzania ili kuonyesha wamekubali asilimia 100 kununua mazao kwa ajili ya chakula.

Alisema wataendelea kufanya ushirikiano na Tanzania katika ununuzi wa mazao ya chakula ili kuhakikisha Congo haipati shida.

## HABARI KITAIFA

# Dawati la teknolojia, ubunifu kuanzishwa

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepanga kuanzisha madawati ya teknolojia na ubunifu kuanzia shule za msingi, ili kukuza na kuibua vipaji na wabunifu wengi nchini.

Mkurugenzi wa Sayansi na Teknolojia wa wizara hiyo, Prof. Ladislaus Mnyone, alisema hayo jana wakati wa mjadala maalumu kati ya Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), waandishi na wahariri wa vyombo vya habari uliofanyika Dar es Salaam.

Prof. Mnyone alisema wako katika mpango wa kuainisha aina ya teknolojia zinazokidhi mahitaji yaliyopo nchini na kwamba lengo ni kuhakikisha teknolojia za kidijitali zinatumika katika sekta mbalimbali, ikiwamo katika kuleta mageuzi sekta ya elimu nchini.

Alisema tayari serikali imekamilisha mkakati wa kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo itakwenda sambamba na matumizi ya sayansi na ubunifu.

Pia alisema wanapanga kushirikisha Watanzania wanaoishi nje ya nchi 'diaspora' katika kukuza sayansi teknolojia na ubunifu kama miongoni mwa mikakati ya kuongeza kasi ya maendeleo katika sekta hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema kaulimbiu ya Wiki ya Ubunifu kwa mwaka huu ni "Ubunifu kwa Maendeleo Jumuishi ya Rasilimali Watu".

"Na tunajivunia mambo mengi yaliyofanyika katika miaka hii 10 tangu tuanze kuwa na wiki ya ubunifu, ikiwamo kutoa fursa na kuongeza uelewa na ali kwa vijana wabunifu ambao pamoja na mambo mengine, wamepata fursa ya kazi zao kuonekana na kufanyiwa kazi,"alisema Dk. Nungu.

# Samia kuwakusanya Dar JK na wastaafu wenzake Afrika

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA inaungana na nchi zingine barani Afrika kuadhimisha miaka 20 tangu kuundwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa kuwakutanisha marais walioko madarakani na wastaafu.

Maadhimisho hayo yatafanyika Mei 25, mwaka huu, jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na Kamisheni ya Afrika na yataongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, aliwaambia waandishi wa habari, jana jijini Dar es Salaam. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni 'Miaka 20 ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika'.

"Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Afrika (AU). Tangu ulipoanzishwa kulifanyika mabadiliko ya muundo na baada hapo kikaundwa chombo cha kusimamia amani na usalama barani Afrika.

"Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, lina wajumbe 15, huteuliwa baada ya muda kwa mzunguko, kukabiliana na migogoro, kusuluhisha mwezi huu wa Mei, Mwenyekiti ni Tanzania," alisema .



Makamba alisema Tanzania ni mhimili wa amani barani Afrika kutokana na nchi kadhaa wakati zikitafuta uhuru na ukombozi wa nchi zao, zilitumia Tanzania kama kituo, kupanga mikakati ya kujikomboa.

"Tanzania inatambulika kwa mchango mkubwa wa ukombozi wetu. Viongozi wengi wa Afrika walioishi hapa kipindi hicho, wanazungumza kiswahili vizuri," alisema Makamba.

"Dhima ya Tanzania, ilibadilika ikawa ni kulinda amani. Tutafanya sherehe Dar es Salaam Rais ameaalika viongozi wa sasa na wastaafu, watakuwapo Joacquim Chissano (Msumbiji), Olusegun Obasanjo (Nigeria), Domitien Ndayizeye (Burundi) na Jakaya Kikwete (Tanzania)," alibainisha.

## TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA NA JAMII

### TAARIFA YA AWALI YA MRADI TARAJIWA WA UZALISHAJI WA GESI YA HELIUM KATIKA WILAYA YA MOMBA, MKOA WA SONGWE

Gogota (Tz) Limited ambayo ni kampuni tanzu ya Helium One Global Limited inamiliki vitalu vya Leseni ya Utafutaji madini (PL) namba PL 10713/2015 chenye Kilomita za Mraba 297.58 na PL 10712/2015 chenye Kilomita za Mraba 264.25 katika eneo la mashariki mwa bonde la Rukwa, kusini mwa Tanzania. Kampuni hii imekamilisha utafiti wa madini mwaka 2023 na imebaini uwepo wa gesi ya Helium. Gesi hiyo inatarajiwa kuwa na kiwango cha kati ya asilimia 4.2 na 10.

Kampuni ya Gogota (TZ) Limited, inatarajia kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii (ESIA) kwa Mradi unaopendekezwa wa uzalishaji wa gesi ya helium kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Kanuni zake na sheria nyingine za Tanzania na Kimataifa. Eneo la Mradi liko katika Wilaya ya Momba ndani ya Mkoa wa Songwe.

Kanuni ya 17(2a) cha kanuni za udhibiti na ukaguzi wa athari za kimazingira ya mwaka 2005, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018, inamtaka muendeleza mradi kutoa taarifa kwa umma kuhusu mradi pendekezwa kwa muda wa wiki mbili mfululizo kwenye chombo cha habari ambacho kinasikika nchi nzima. Kwa mantiki hiyo taarifa hii inawasilishwa kuufahamisha umma kwamba kampuni ya MTL Consulting Limited imepewa kazi ya kufanya tathimini ya athari za uzalishaji wa gesi ya helium kwenye mazingira na jamii kwa niaba ya kampuni ya Gogota (TZ). Tathmini hii itafanyika katika kata tatu zitakazojumuisha vijiji tisa ambavyo ni Kamsamba, Muungano, Kasanu, Mpapa, Masanyita, Itumbula, Lwatwe, Samang'ombe na Mkonko.

Taarifa hii imetolewa kuomba maoni na mapendekezo ya wadau au pande zozote ambazo kwa namna moja au nyingine wanaweza kuathiriwa na mradi huu. Mtu yeyote mwenye maslahi, maoni, wazo au maarifa (ufahamu) kuhusu athari zozote za kimazingira na kijamii za mradi pendekezwa anaweza kuwasiliana au kuwasilisha maoni yake kwa maandishi kwa anwani zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| Mkurugenzi<br>Helium One (Gogota) Limited.<br>Gorofa ya Pili, Kilwa House, 369 Toure Drive, Oyster Bay<br>S.L.P 62, Dar Es Salaam, Tanzania<br>Mawasiliano: 0682 636 828<br>Barua pepe:gogota@helium-one.co.za | Mkurugenzi Mkuu,<br>Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),<br>S.L.P 63154, Regent Estate, Dar es Salaam, Tanzania.<br>Mawasiliano: +255 22 2774889<br>Barua pepe: nemc@nemctz.org | Meneja Mkuu<br>MTL Consulting Limited,<br>Victoria House, Gorofa ya tisa, Kitalu Na. 37, Regent Estate, Barabara mpya ya Bagamoyo,<br>S.L.P 77894, Dar es Salaam.<br>Simu ya mezani: +255 22 2926117,<br>Simu ya mkononi:+255 767360225/743127611<br>Barua pepe: info@mtlconsultingtz.com |

## TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA NA JAMII

### TAARIFA YA AWALI YA MRADI TARAJIWA WA UZALISHAJI WA GESI YA HELIUM KATIKA WILAYA YA MOMBA, MKOA WA SONGWE

Njozi (Tz) Limited ambayo ni kampuni tanzu ya Helium One Global Limited inamiliki vitalu vya Leseni ya Utafutaji madini (PL) namba PL 10713/2015 chenye Kilomita za Mraba 297.58 na PL 10712/2015 chenye Kilomita za Mraba 264.25 katika eneo la mashariki mwa bonde la Rukwa, kusini mwa Tanzania. Kampuni hii imekamilisha utafiti wa madini mwaka 2023 na imebaini uwepo wa gesi ya Helium. Gesi hiyo inatarajiwa kuwa na kiwango cha kati ya asilimia 4.2 na 10.

Kampuni ya Njozi (TZ) Limited, inatarajia kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii (ESIA) kwa Mradi unaopendekezwa wa uzalishaji wa gesi ya helium kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Kanuni zake na sheria nyingine za Tanzania na Kimataifa. Eneo la Mradi liko katika Wilaya ya Momba ndani ya Mkoa wa Songwe.

Kanuni ya 17(2a) cha kanuni za udhibiti na ukaguzi wa athari za kimazingira ya mwaka 2005, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018, inamtaka muendeleza mradi kutoa taarifa kwa umma kuhusu mradi pendekezwa kwa muda wa wiki mbili mfululizo kwenye chombo cha habari ambacho kinasikika nchi nzima. Kwa mantiki hiyo taarifa hii inawasilishwa kuufahamisha umma kwamba kampuni ya MTL Consulting Limited imepewa kazi ya kufanya tathimini ya athari za uzalishaji wa gesi ya helium kwenye mazingira na jamii kwa niaba ya kampuni ya Njozi (TZ). Tathmini hii itafanyika katika kata tatu ambazo ni Mpapa, Ivuna na Kamsamba zitakazojumuisha vijiji vya Kipeta, Kilangawana, Kilyamatundu, Mkonko, Usoche, Mpapa, Mkuyu, Senga, Kamsamba, Itumbula, Samang'ombe, Lwatwe, Mpapa, Kasanu na Masanyita.

Taarifa hii imetolewa kuomba maoni na mapendekezo ya wadau au pande zozote ambazo kwa namna moja au nyingine wanaweza kuathiriwa na mradi huu. Mtu yeyote mwenye maslahi, maoni, wazo au maarifa (ufahamu) kuhusu athari zozote za kimazingira na kijamii za mradi pendekezwa anaweza kuwasiliana au kuwasilisha maoni yake kwa maandishi kwa anwani zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| Mkurugenzi<br>Helium One (Njozi) Limited.<br>Gorofa ya Pili, Kilwa House, 369 Toure Drive, Oyster Bay<br>S.L.P 62, Dar Es Salaam, Tanzania<br>Mawasiliano: 0682 636 828<br>Barua pepe: njozi@helium-one.com | Mkurugenzi Mkuu,<br>Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),<br>S.L.P 63154, Regent Estate, Dar es Salaam, Tanzania.<br>Mawasiliano: +255 22 2774889<br>Barua pepe: nemc@nemctz.org | Meneja Mkuu<br>MTL Consulting Limited,<br>Victoria House, Gorofa ya tisa, Kitalu Na. 37, Regent Estate, Barabara mpya ya Bagamoyo,<br>S.L.P 77894, Dar es Salaam.<br>Simu ya mezani: +255 22 2926117,<br>Simu ya mkononi: +255 767360225/743127611<br>Barua pepe: info@mtlconsultingtz.com |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watendaji, watumishi watambue wajibu wao

**KWA** muda mrefu viongozi wa kitaifa wanapotembelea mikoa kukagua shughuli za maendeleo au kufanya ziara za kikazi, wamekuwa wakikutana na kero mbalimbali zinazowahusu wananchi katika sekta anuai kama vile ardhi, afya, elimu na miundombinu.

Kadhalika, viongozi wa ngazi za mikoa kama vile wakuu wa mikoa, wanapofanya ziara kama hizo kwenye wilaya na halmashauri, hali imekuwa vivyo hivyo ya wananchi kulalamikia kero kwenye sekta zinazogusa maisha yao ya kila siku. Wananchi wengine wamekuwa wakilalamika hali ngumu ya maisha ambayo huenda makali yake yangepungua kama watendaji katika ngazi husika wangetimiza wajibu wao.

Uwapo wa matatizo na kero hizo inadhihirisha kwamba viongozi na watendaji waliopewa majukumu ya kusimamia sekta hizo katika ngazi husika ama hawatimizi wajibu wao, hawajui yawapasayo kutenda au wamejenga na kuendeleza dhana kwamba wamepata nafasi hiyo kwa maslahi binafsi.

Mambo kama hayo yamebainika muda mrefu baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kuibua madudu katika ziara walizozifanya, hivyo kudhihirika wazi kwamba waliopewa nafasi hizo ni mzigo mzito usioweza kubebeka. Wameshindwa kutatua kero zinazowakabili wananchi na baadhi yao kugeuka sehemu ya kuwakandamiza wananchi kwa kujinufaisha kupitia nafasi zao.

Baada ya viongozi hao wakuu kubaini hayo na kuchukua hatua dhidi ya wahusika ikiwamo uteuzi wao kutenguliwa, hali imekuwa hiyo hiyo baada ya maeneo kadhaa kuonekana matatizo kama hayo bado yanaendelea.

Hivi karibuni, kwa mfano, wakuu wa mikoa ya Arusha, Paul Makonda, na mwenzake wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, walifanya ziara na kubaini madudu kama hayo yakiendelea tena hata kuzidi. Makonda katika kliniki aliyoifanya mkoani Arusha, alikutana na kero za muda mrefu ambazo hazijapatiwa majawabu na watendaji hadi kuingilia kati na baadhi kutatuliwa mbele yake tena kwa muda mfupi.

Dk. Nawanda naye mapema wiki hii, alifanya ziara ya kushtukiza katika wilaya ya Busega na kubaini kuwa jenereta lililotolewa na Wizara ya Afya kwa ajili ya hospitali ya wilaya, halijatumika kwa zaidi ya mwaka kutokana na kukosekana kwa kilo tano za chumvi, makopo mawili ya mkaa na lita 15 za dizeli.

Kutokana na kuwapo kwa tatizo hilo, Dk. Nawanda aliwaagiza mkuu wa wilaya na mkurugenzi mtendaji wa halmashauri kutatua kero hiyo ndani ya siku tano ili kuwezesha kifaa hicho kufanya kazi na hatimaye kuimarisha huduma za tiba ambazo zimekuwa zikizorota pindi umeme unapokatika.

Mambo kama hayo yamezua maswali magumu yasiyo na majibu ikiwamo kama viongozi wa ngazi mbalimbali wanatambua wajibu wao katika utumishi wao. Hivi ni mpaka Rais, makamu wake, Waziri mkuu au wakuu wa mikoa wafanye ziara ndipo matatizo ya wananchi yatatuliwe?

Watendaji katika wilaya, halmashauri wanafanya nini mpaka matatizo hayo kuwa mengi na kusababisha taabu kwa wananchi? Walioteuliwa kutekeleza majukumu kisekta wanatambua wajibu wao au wanadhani wamewekwa hapo kwa ajili ya ulaji?

Ni wakati mwafaka sasa kwa serikali kuangalia mfumo mpya au kufanya utafiti kuhusu njia nzuri ya kuwapata watendaji ambao watakuwa chachu katika kutatua kero za wananchi na kuleta maendeleo katika ngazi za chini hususan wilaya na halmashauri. Mifano iliyotolewa inaonyesha kwamba wengi hawana uwezo au hawatambui wajibu wao.

Wananchi wanahitaji kutatuliwa kero zao, hivyo ni wajibu wa watendaji kuanzia wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri pamoja na wakuu wa idara kujitambua kuhusu wajibu wao na hatimaye kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Kuna wazazi wanawakodia watoto usafiri wa shule wenye kasoro wasizozijua

**HADI** sasa kwa kiasi gani nchi yetu ilikofikia katika baadhi ya huduma za kijamii ndani ya uchumi wa soko, tukiri kuna hatua imepigwa kulinganisha na tulikotoka.

Katika shule zilizoko kuna za umma na binafsi (kulipia). Niseme huko kwenye shule za kulipia, kuna taratibu za utoaji huduma zinazoendana na gharama, wazazi na walezi wanawajibika nazo kwa niaba ya watoto wao.

Serikali nayo inapaswa kwenda na mabadiliko ya mahitaji hayo, ikiweka sheria, kanuni na mwenendo kusimamia hayo. Hapo kuna huduma za usafiri.

Lakini, katika utekekezaji wake, kumeibuka malalamiko kwamba, kuna tabia za baadhi ya shule, zinatoa huduma hizo, huku zikiipa kisogo sheria, miongozi na taratibu za usalama barabarani.

Msingi uliowekwa kiserikali, unawataka wasafarishaji kuzingatia sheria kupitia vyombo vyao vya moto.

Lakini, katika uhalisi wa utekelezaji, ukiangalia kwa sasa kuna baadhi ya shule na hasa mijini ambako shule hizo ndio zimetapakaa, masuala ya usafiri wa wanafunzi wao hawayazingatii, pia usalama wao, wanachokiangalia ni kuchukua oda ya usafiri.

Ukiangalia, kuna shule zinatoa huduma ya usafirisaji, lakini kinachosikitisha ni kwamba, unakuta watoto walio katika gari hizo tena wadogo, wamejazana huku wengine wakiwa wamebebana.

Kuanzia hapo, tayari ni hali inayokiuka sheria,kwani idadi ya abiria katika gari inajulikana.

Lingine ni kwamba, pia unakuta kuna walimu nao wapo katika magari hayo wamekaa katika viti bila ya kuwaonea huruma watoto hao, ambao ndio wenye haki kisheria.

Hapo ina maana kwamba, sehemu ya mkataba kati ya shule nao, kupitia wazi na walezi wao ni kwamba wamesajiliwa na wagharamia huduma yenyewe kupitia wanaowalea.

Kuna wazazi ambao watoto wao hawatumii usafiri wa shule na kuamua kuwatafutia usafiri ama wa kama wa kukodi, ili waende shule na wengine wanatembea, kutegemea umbali wa sehemu wanayotoka.

Inawezekana kwa wazazi hao, kuna wazazi wanaona gharama za usafiri wa shule ni juu na wanaamua mbadala wa usafiri binafsi.

Kwa sehemu kubwa, wazazi wanaokwepa ni pesa za usafiri wa shule kuwa kubwa. Lakini, haimaanishi kwamba, huko kwenye mabdala kuna manufaa zaidi. Inategemea!

Ukweli unaotawala, pamoja na wazazi kukwepa usafiri wa shule, ieleweke vilevile si nafuu. Wazazi hao wanashindwa kuelewa, hata huo mbadala wao wa usafiri binafsi, nao una changamoto zake.

Kuna baadhi ya gari zinajaza abiria watoto na huwezi amini idadi yao, pale wanaposhuka shule au kurudi majumbani.

Yaani hizo gari za binafsi nyingi zinazobeba Watoto, huwa na vioo vya 'tinted' huwajaza watoto wanaposhushwa shule, ndio hapo utakaposhangaa idadi ya watoto wanaoshuka humo.

Au unakuta gari hiyo ya binafsi, imepata tatizo barabarani, ndipo hapo utaona watoto wanatoka katika hiyo gari wapo wengi.

Hilo ni jukumu la wazazi kujiridhisha na huo usafiri wanaoukimbilia binafsi uko salama?

Inawezekana mzazi anakuwa hajui na ndio sababu mzazi huyo analipia usafiri huo, lakini ajali inapotokea, ndio hapo wazazi hushituka pale wanapoambiwa idadi ya wanafunzi iliyokuwa katika gari hiyo inatisha.

Pia, katika usafiri binafsi, wapo wanaozingatia usalama wa watoto na wapo wasiozingatia na kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi, huku gari uwezo wake ukiwa mdogo.

Katika usafiri wa shule, baadhi ya usafiri huo, hauzingatii masuala ya watoto, ambako magari hujaza watoto, huku wengine wamekumbatia, lakini cha kushangaza unakuta walimu wamekalia viti.

Naamini wanafunzi wanalipiwa usafiri na wazazi, lakini walimu wao 'hudowea' kupanda gari la wanafunzi, sidhani kama hata wanalipia usafiri huo.

Hivyo, inatakiwa haki za wanafunzi izingatiwe na sio kuwajaza wanafunzi katika gari hata kupumua au kujinyoosha mikono wanashindwa.

# Malasusa: Kuna shida kubwa uandikaji wosia

**Na Grace Gurisha**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Kiinjili na Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Alex Malasusa amewataka wananchi kuandika wosia ili kupunguza kesi za mirathi mahakamani.

Amesema kesi hizo hivi sasa ni nyingi mahakamani na zimekuwa zinaacha maumivu makubwa kwa familia.

Vilevile, Kituo Jumuishi cha Masuala ya Familia kilichopo Temeke, Dar es Salaam chenye Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama Kuu kikibainisha kuwa kuanzia Januari hadi Aprili mwaka huu, kimetoa hati za talaka 444, hali ambayo inaonesha kuna shida katika familia nyingi.

Askofu Malasusa alitoa kauli hiyo baada ya kutembelea kituo hicho jijini Dar es Salaam juzi akiwa ameongozana na wakuu wa majimbo yote sita ya Dayosisi ya Mashariki na Pwani na wachungaji, wakiongozwa na wenyeji wao Jaji Mfawidhi wa kituo hicho, Mwanabaraka Mnyukwa na Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Frank Moshi.

"Mtu anapoacha wosia, si suala la kujichulia, Askofu Malasusa alisema. Tumekuwa na tabia tukidhani mtu akiacha wosia kama vile anataka kufa kumbe ni kitu kizuri ambacho kitapunguza ugomvi usio na maana.

Sisi kama viongozi wa dini tunatakiwa kukumbusha na kuhamasisha waumini waliyo chini yetu ili waweze kuweka utaratibu mzuri kwa ajili ya kupunguza migogoro ya kifamilia.

Masuala ya ndoa, mirathi yanaacha maumivu sana katika familia nyingi, ninaamini wachungaji waliofika hapa leo (juzi) watafanya hivyo."

Askofu huyo alisema kupitia ziara hiyo wamejifunza mambo mengi ambayo kimsingi, ukiyafuatilia unaona ni kazi zao za kila siku wanazofanya viongozi wa dini.

"Kwa mfano, tumejifunza kwamba upo msaada wa kisheria kwa watu ambao wanakosa nguvu ya kifedha ya kuweka mawakili, lakini tumekuta ustawi wa jamii ambao wao pamoja na mambo mengine wanatoa ushauri na wakati mwingine wanashauri watu kuondoa kesi mahakamani na kuwapatanisha," alisema.

Pia alisema jambo la kipekee katika mahakama hiyo ni kuweka kitengo cha mahakama ya watoto. Huko watoto nao wanapewa nafasi ya kupata haki zao kwa kuwatengea sehemu yao.

Jaji Mnyukwa alisema kituo hicho kinahusika moja kwa moja na utatuzi wa masuala ya familia na katika utatuzi huo mahakama pekee isingeweza ndiyo maana wanashirikiana na wadau mbalimbali, wakiwamo viongozi wa dini.

"Kituo chetu kwa takwimu kwa kipindi cha Januari hadi Aprili mwaka huu kiliweza kutoa jumla ya hati za talaka 444. Ukiangalia wingi wa idadi ya ndoa ambazo zinavunjwa katika kituo hiki, tunawaomba mwendelee kuzungumza na waumini wenu kabla hawajafika mahakamani ili kupunguza tatizo hili," alisema Jaji Mnyukwa.

Ofisa Ustawi wa Jamii katika kituo hicho, Alfred Mvungi, aliomba viongozi wa dini kuongeza muda wa mafunzo ya ndoa kanisani; iwe hata miezi kadhaa kwa kuwa migogoro mingi wanayokutana nayo inaonekana mafunzo ya muda mrefu yanahitajika.

"Tunaomba mwendelee kuziombea familia, kesi nyingi tunazokutana nazo ni za migogoro ya ndoa, kinababa wanakuwa hawatekelezi majukumu yao, wanayakimbia na kuwaachia kinamama.

"Kuna kinababa wanaofanya vizuri katika malezi, huwa wanawaleta wake zao hapa kwa kushindwa kulea watoto," alisema Mvungi.

## Aliyesotea haki kazini kwa miaka 32 kulipwa mil. 207/-

**Na Kulwa Mzee**

MFANYAKAZI wa Kampuni ya Saruji Tanga, Ephraim Joram, ameshinda rufani dhidi ya mwajiri wake na Mahakama ya Rufani Tanzania imebariki alipwe malimbikizo ya mishahara yake ya miaka 32, jumla Sh. milioni 207 kama ilivyoamuliwa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Dar es Salaam mwaka 2017.

Uamuzi huo wa Mahakama umetolewa mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji Rehema Mkuye, Barke Sahel na Abraham Mwampashi.

Mahakama katika uamuzi wake ilisema mshahara wa Sh. 500,000 kwa mwezi ulithibitishwa na CMA, hivyo baada ya kupitia shauri hilo iliona rufani ina msingi, iliondoa uamuzi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi na kuamuru uamuzi wa CMA utekelezwe.

"Joram alifikisha shauri kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi mwaka 2006 na hadi anafikia hatua hiyo alikuwa mfanyakazi halali wa Kampuni ya Saruji Tanga.


"Anastahili kulipwa mshahara wa Sh. 500,000 kwa mwezi mara miezi 12 mara miaka 32, jumla Sh. milioni 192.

"Mlalamikaji anastahili kulipwa nauli ya kwenda likizo Sh. 15,500,000 na michango mingine lazima izingatiwe ambapo jumla kuu alipwe Sh. 207,500,000," ilisema tume katika uamuzi wake.

Malipo hayo yalitakiwa kulipwa ndani ya siku 30 na upande usioridhika ulielekezwa kuomba marejeo. Mlalamikaji alikuwa mfanyakazi wa kampuni hiyo tangu mwaka 1985 na kwamba aliachishwa kazi bila kufuata taratibu za kisheria.

Baada ya uamuzi huo wa CMA, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Saruji Tanga aliwasilisha maombi ya marejeo Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kuomba uamuzi ufanyiwe marejeo. Shauri hilo lilikuwa mbele ya Jaji Moses Mzuna ambaye baada ya kufanya marejeo mwaka 2019, mahakama iliona kwamba uamuzi kwamba mlalamikaji alipwe mishahara ya miaka 32 na malipo mengine haukuwa sawa.

Mahakama hiyo ilisema mlalamikaji aliajiriwa mwaka 1985, mwajiri alishindwa kutoa ushirikiano, hivyo iliona mlalamikaji alistahili kulipwa mishahara ya miezi 12 kama ilivyowahi kuamuliwa na Mahakama ya Kisutu mwaka 2005.



Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, Deo Mwanyika (kulia) akijadiliana jambo na Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTILINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAIN | INTERCITY BULIDERS LIMITED | NYUMBA ZILIZOPO KWENYE SHAMBA KIWANJA NAMBA 675, HATI NAMBA 39900 | INTERCITY BULIDERS LIMITED | CHANGANYIKENI -DAR ES SALAAM | 7/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | INTERCITY BULIDERS LIMITED | 1. GARI ROAD ROLLER T423 DBV 2.GARI, TRAILER T984 DAH | INTERCITY BULIDERS LIMITED | KURASINI | 10/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | LILIAN CLAUDY KANJE | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 145001,KIWANJA NA.101 KITALU 'D' | LILIAN CLAUDY KANJE | KIGOGO- MANISPAA YA KINONDONI | 06/06/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 07/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MTIBU FISH ENTERPRISES | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.DSMT1026616, BONYOKWA | HAMISA BAUSI ABUU | KIMARA BONYOKWA | 07/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | DOMINICK LINUS MAIKO | NYUMBA (3) | 1.DOMINICK LINUS MAIKO 2.DOMINIC LIVING SHIO 3.SYLVESTER APOLINARY MBOYA | 1.NZASA- CHARAMBE 2.KIBADA KIGAMBONI 3.MBEZI MSUMI | 10/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ZAWADI JUMA KWALAZI | NYUMBA | ZAWADI JUMA KWALAZI | SALA SALA-WAZO | 13/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933/0759282344/0715868000**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# Sheria mpya ya Ndoa yanukia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UANDAAJI muswada wa marekebisho ya Sheria ya Ndoa uko katika hatua za ndani serikalini na zitakapokamilisha utawasilishwa bungeni.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Thea Ntara aliyetaka kujua lini serikali itawasilisha bungeni muswada huo ili kuunga mkono vita dhidi ya ndoa za utotoni.

Sagini alisema kuwa baada ya uamuzi wa mahakama juu ya kesi iliyofunguliwa kupinga umri wa kuolewa uliopo kisheria, serikali iliwasilisha bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa kupitia Tangazo Na 1. Vol 102 la tarehe 5 Februari, 2021 kwa kupendekeza umri wa kuoa au kuolewa uwe kuanzia miaka 18.

Alisema Bunge kupitia Kamati ya Uongozi lilielekeza serikali kukusanya maoni ya wananchi kuhusiana na suala hilo na imetekeleza.

Vilevile, alisema kuwa Aprili 26, 2023, serikali ilifanya Kongamano la Sheria ya Ndoa jijini Dodoma ili kupata maoni zaidi juu ya umri wa kuingia katika ndoa.

Alisema kongamano hilo lilikuwa na ushirikishwaji mpana wa wadau mbalimbali wakiwamo wazee wa kimila, viongozi wa dini, wanataaluma, wanafunzi wa ngazi mbalimbali, watu mashuhuri na wabunge.

Alifafanua kuwa kongamano hilo lilikuwa mbashara kupitia Televisheni ya Taifa na wananchi waliruhusiwa kupiga simu na kutoa maoni yao.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Esther Maleko alitaka kujua mkakati wa serikali kuimarisha huduma za usuluhishi kwa migogoro ya ndoa na haki za watoto.

Akijibu swali hilo, Sagini alisema kwa mujibu wa kifungu cha 102 cha Sheria ya Ndoa, Sura 29, waziri mwenye dhamana na masuala ya sheria amepewa mamlaka ya kuanzisha Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa katika kila kata au sehemu nyingine yeyote atakayoona inafaa.

Alisema mabaraza hayo yameanzishwa na yanafanya kazi katika kata zote nchini na kifungu cha 101 cha Sheria ya Ndoa kinaelekeza mgogoro wowote wa ndoa lazima upitie katika hatua ya usuluhishi kabla ya kuwasilishwa mahakamani.

Kuhusu uboreshaji Sheria ya Ndoa ambayo masuala ya fidia kwa matunzo ya watoto yanafanyika, Naibu Waziri huyo alisema sheria hiyo ni ya muda mrefu, hivyo viwango vilivyokuwa vimewekwa vimepitwa na wakati huku akielekeza Tume ya Marekebisho ya Sheria kuzingatia viwango hivyo ili kwenda na wakati.



Takataka za chupa tupu za plastiki zikiwa zimetupwa kwenye mtaro wa maji ya mvua kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la mataa ya kona ya ITV Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana. Baadhi ya mamalishe na wafanyabiashara wa maduka wa eneo hilo, wanao wajibu wa kuufanyia usafi mtaro huo kutokana na kuwa taka hizo zinatupwa na wateja wa bidhaa wanazoziuza.**PICHA: JOHN BADI**

# Walia na ushiriki mdogo wa wanawake

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

USHIRIKI wa wanawake kwenye uchaguzi uko chini na hivyo kusababisha kundi hilo kuwa na wawakilishi wachache kwenye mamlaka za uamuzi nchini.

Kutokana na hali hiyo uhamasishaji unatakiwa kufanyika kuanzia ngazi ya kijiji/mtaa ili katika uchaguzi ujao idadi ya viongozi wanawake iongezeke.

Rai hiyo ilitolewa jana Chalinze wakati wa kikao kazi cha kujadili shughuli za asasi zinazojishughulisha na masuala ya wanawake, kikijumuisha maofisa maendeleo ya jamii kutoka Halmashauri za Kibaha Mjini, Chalinze na Kisarawe kilichoandaliwa na Shirika la Un Women.

Katika kikao kazi hicho, Mwakilishi wa Un Women, Deogratias Mamiro alisema nguvu zaidi kupata viongozi wanawake inatakiwa kuwekwa kuanzia kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka unaotarajiwa kufanyika mwaka huu

Mamiro alieleza kuwa kati ya Wenyeviti wote wa Serikali za Mitaa na Vitongoji nchini, wanawake ni asilimia 12 tu huku kukiwa na asilimia 6.5 ya madiwani wanawake waliochaguliwa na asilimia 27 ya Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa nchini.

Alisema kupitia mradi unaotekelezwa na shirika hilo ambao unalenga kuhakikisha ushiriki wa wanawake katika uongozi unaongezeka, wadau kutoka asasi zinazotekeleza mradi huo watakuwa na wajibu wa kushuka kwa jamii na kuhamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi.

Mradi huo ambao unatekelezwa katika mikoa sita na halmashauri 18 nchini unalenga kuleta matokeo ya kitaifa na kimataifa kwa kufikia asilimia 50 kwa 50 kwenye ngazi za uongozi.

Awali akifungua kikao kazi hicho, Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani, Rashid Mchata, alisema serikali inahakikisha wanawake wanashiriki katika vyombo mbalimbali vya uamuzi.

Alipongeza Un Women kwa namna inavyoshirikiana na serikali kutekeleza miradi yake huku akisema mkoa huo unasimamia wanawake kushiriki katika mambo mablimbali ya uongozi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Pwani, Grace Tete alisema katika kuandaa bajeti ya mkoa huo, serikali imeendelea kuzingatia masuala ya kijinsia katika bajeti zake.

Grace pia alisema wanaendelea kufuatilia majukwaa ya uwezeshaji yaliyoanzishwa kama yanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia malengo. Mazingira wezeshi kwa wanawake na watoto wa kike yameendelea kuwekwa Ili kuwainua kiuchumi.

# Neema yanukia bima ya mifugo, usalama chakula

**Na Mary Geofrey**

WAFUGAJI nchini wanatarajiwa kunufaika na makubaliano ya kukuza bima ya kilimo, hasa bima ya mifugo yaliyoingiwa kati ya Kampuni ya Bima ya CRDB na ACRE Africa.

Ushirikiano wa taasisi hizo unaashiria hatua muhimu katika juhudi zao za pamoja kuunga mkono sekta ya kilimo na kuboresha usalama wa chakula katika ukanda.

Katika taarifa yake kwenye hafla ya kutia saini makubaliano hayo iliyofanyika makao makuu ya CRDB Insurance Company jijini Dar es Salaam jana, Wilson Mnzava, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Insurance Company, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano huo.

"Moja ya changamoto kuu zinazokabili Afrika leo ni usalama wa chakula. Vitisho vinavyosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa vinaendelea kuvuruga uzalishaji wa chakula na kusababisha hatari kubwa kwa maisha ya mamilioni ya wakulima na wafugaji.

"CRDB Insurance Company tunatambua uharaka wa changamoto hizi na tumejipanga kutoa suluhisho zinazowaunga mkono wakulima wetu na mifugo yao katika kukabiliana na hali hizi zisizo na uhakika," alisema Mnzava.

Aliutaja mpango huo unasadifu Mpango wa Serikali wa Kukuza Sekta ya Fedha 2020-2030, ambao unalenga kuwa na angalau asilimia 50 ya watu wazima kuwa na bima moja.

Alisema kampuni za bima zinahimizwa kubuni suluhisho za bima zinazokidhi mahitaji ya wateja na CRDB Insurance Company iko mstari wa mbele katika mpango huo, ikitoa bidhaa za bima za kilimo zenye ubunifu, ikiwamo bima ya mifugo.

Kampuni imejizatiti kutekeleza mkakati wa kundi na kukuza kilimo nchini. Mnzava alibainisha kwamba, "Kwa kutumia mtandao wetu mkubwa wa matawi ya benki yetu na mawakala, tunaweza kufanya huduma hizi muhimu za bima zipatikane kwa wananchi wetu.

"Ahadi yetu ni kuhakikisha kuwa wakulima kote nchini wanapata msaada wanaohitaji kulinda maisha yao na kuchangia usalama wa chakula wa taifa."

Alisema ushirikiano na ACRE Africa unawakilisha muungano wa kimkakati wa kuunga mkono ajenda ya serikali na kutoa suluhisho kamili za bima zinazokidhi mahitaji ya sekta ya kilimo.

"Ushirikiano huu unaashiria maono yetu ya pamoja ya jamii ya kilimo inayojitegemea na Tanzania yenye ustawi," aliongeza Mnzava.

"Kampuni yetu inatoa shukrani zake kwa wadau wote ambao wamechangia kufanikisha ushirikiano huu. Tunapoendelea mbele, tumejipanga kufanya kazi pamoja kulinda usalama wa chakula wa taifa na kuwaunga mkono wakulima na wafugaji wenye bidii ambao ni uti wa mgongo wa uchumi wetu," aliongeza.





## Aweso amteua Mwakatobe mjumbe AUWASA

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso amemteua Christine Mwakatobe kuwa mjumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA), kuanzia Mei 13 mwaka huu.

Mwakatobe kwa sasa ni Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), aliteuliwa mwaka huu na Rais Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo.

Sehemu ya barua ya uteuzi huo inaeleza kuwa, Waziri Aweso, amemteua Mwakatobe kwenye bodi hiyo, nafasi ya mwakilishi wa watumiaji wakubwa wa maji jijini Arusha.

"Ni matarajio yangu kuwa utaupokea uteuzi na kufanya kazi kwa bidii na uadilifu ili Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha, iendelee kutoa huduma bora na zenye viwango vya hali ya juu," alisema Waziri Aweso.

Katika barua hiyo, Waziri Aweso, alinukuliwa na kusisitiza kuwa Mwakatobe, atatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya wizara, Msajili wa Hazina na serikali.

Kabla ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa AICC, Machi mwaka huu, Mwakatobe ambaye kitaaluma ni mchumi na mtaalamu wa masoko, alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji na Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KADCO).

## Madaktari bingwa 30 kutoa matibabu Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

MADAKTARI bingwa na wabobezi wa magonjwa mbalimbali 30 wamepiga kambi kwa siku nne wilayani Muheza mkoani Tanga, kwa ajili ya kutoa huduma.

Lengo la madaktari hao kuweka kambi hiyo ni kuwapunguzia gharama wananchi za kufuata huduma za kibingwa na ubingwa mbali na makazi yao.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah, baada ya uzinduzi wa huduma ya mkoba ya madaktari bingwa wa Rais Samia Suluhu Hassan katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza.

Hata hivyo, alisema wananchi wanapatiwa huduma na madaktari hao ikiwa ni sehemu ya utoaji huduma kwenye kambi ya matibabu ya kibingwa inayofanyika katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza iliyopo Kijiji cha Lusanga.

Alisema kambi hiyo imeonekana kuwa na tija kwa wananchi, imepunguzia gharama za kufuata huduma nje ya wilaya.

Hivyo, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapelekea madaktari bingwa mkoani Tanga na kwa upekee katika wilaya hiyo.

Pia, aliwakaribisha wakazi wa Muheza kujitokeza kwa wingi katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza (Mama Samia District Hospital), kwa ajili ya kupata huduma zote muhimu za kimatibabu.

# Sendiga awashukia wazazi wanaowatumikisha watoto

**Na Allan ISACK,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, ametoa onyo kwa wazazi na walezi mkoani hapa kuacha tabia ya kuwafanyisha shughuli za nyumbani na kuchunga mifugo watoto, badala yake amewataka wawapeleke shule.

Alitoa onyo hilo Kijiji cha Emboreet wilayani Simanjiro, baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Kituo cha Mafunzo, Ujuzi na Malezi kwa wasichana, kinachojengwa kwa ufadhili wa Taasisi ya ECLAT Foundation, wakishirikiana na Taasisi ya Upendo kutoka Ujerumani.

Sendiga alisema baadhi ya watoto hasa wa kike wilayani Simanjiro wananyimwa fursa ya elimu na kuozeshwa wakiwa wadogo, akisema ukimwelimisha mtoto wa kike umeielimisha familia na jamii.

"Watoto wa kiume wapewe elimu wasipewe kazi ya kuchunga mifugo wangali wadogo na watoto wa kike wasiozeshwe wakiwa wadogo ila wapatiwe elimu," alisema Sendiga.

Licha ya kuzungumza hayo, alikemea vitendo vya ukatili wa aina mbalimbali ambavyo vinaendelea kuripotiwa kutokea wilayani humo ikiwamo ukeketaji, ubakaji, ulawiti na vipigo.

Pia, aliishukuru familia ya Peter Toima ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya ECLAT Foundation kwa uzalendo walioufanya na kuwa mfano wa kuigwa kwa kutoa eneo lao kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho.

Toima ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Manyara, alisema ECLAT imetengeneza miundombinu mbalimbali katika sekta ya elimu.

Alisema shirika hilo limejenga na kukarabati shule za msingi na sekondari kwenye Wilaya ya Simanjiro na mikoa ya Arusha, Mtwara na Lindi.

Mmoja wa mkazi wa Emboreet ambaye ni mfugaji, Naishok Mollel alisema Toima amekuwa alama kubwa ya elimu katika Wilaya ya Simanjiro.

Alisema jamii ya wafugaji wamekuwa na mwamko mkubwa wa kupenda elimu kutokana na miundombinu inayotengenezwa na shirika hilo.

Ujenzi wa kituo hicho ulianza Mei 18 mwaka 2024 na utagharimu cha Sh. bilioni 1.6 hadi kukamilika kwake.




Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, Priscus Tarimo (wa pili kushoto), akikagua maendeleo ya ujenzi wa kituo cha polisi katika kata ya Karanga, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki, kinachojengwa kwa nguvu za wananchi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Watumishi sita Halmashauri Hai wafutwa kazi kisa utoro

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAFANYAKAZI sita kutoka Idara ya Afya ya Halmashauri ya Hai mkoani Kilimanjaro wamefutwa kazi baada ya kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kutoa huduma kwa wananchi.

Uamuzi wa kuwafukuza kazi ulifikiwa jana na Baraza la Madiwani la Wilaya hiyo, lililoketi katika kikao cha kawaida cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2023/24.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Edmund Rutaraka, alitangaza uamuzi huo wakati akifunga kikao hicho.

"Tumefikia hatua ya kuwafukuza baada ya kujiridhisha watumishi hao (anawataja majina), hawakuwa kazini kwa muda wa mwaka mmoja, kitu ambacho ni kinyume na Sheria ya Utumishi wa Umma," alisema na kuongeza:

"Baraza liligeuka kuwa kamati ya nidhamu kwa ajili ya kuwajadili watumishi saba ambao walitafutwa kwa njia mbalimbali bila mafanikio. Na kamati iliyoundwa ilitoa mapendekezo yao kuwa watumishi hao waondolewe kazini, kwa sababu wemejifukuzisha kazi kwa kutokuwepo kazini".

Alisema mmoja wa watumishi hao kamati imependekeza arudi kazini kutokana na taarifa zake kuonesha kuwa aliomba ruhusa ya kwenda kusoma.

Katika kikao hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Hai, Dionis Myinga, alisema kabla ya kufikia Juni 30 mwaka huu, wamefanikiwa kukusanya mapato kwa asilimia 89.9.



# Wauguzi matatani wakidaiwa kumuomba rushwa mjamzito

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAHUDUMU katika Kituo cha Afya cha Ngaya kilichopo katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga wanatuhumiwa kuomba rushwa ya Sh.150,000 kutoka kwa familia ya mama aliyejifungua mtoto kituoni hapo.

Mkono wa mtoto wa mama huyo ulibainika umevunjika, hivyo wahudumu hao walimuomba kiasi hicho cha fedha ili wamtibu.

Madai hayo yametolewa juzi na mama huyo aliyejifungua, Sophia Budeba na kueleza kuwa licha ya kuombwa kiasi hicho cha fedha awali alipofika kituoni hapo aliombwa pia Sh.40,000 kwa ajili ya kupatiwa huduma ya kujifungua.

Sophia alisema baada ya kutoa kiasi hicho Mei, 18 alipatiwa huduma lakini wakati wa kujifungua mtoto alikuwa ametanguliza mabega hali ambayo ilisababisha mkono kuvunjika wakati akizaliwa.

"Baada ya mkono huo wa kulia kuvunjika tuliombwa Sh. 150,000 kwa ajili ya mtoto huyo kufungwa POP na baada ya hapo alipewa rufani Kwenda Hospitali ya Halmashauri," alisema Sophia.

Muuguzi Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Magreth Kiyenze, alikiri mtoto huyo kupatiwa rufani baada ya kugundulika kuvunjika mkono wakati wa kuzaliwa kwa ajili ya matibabu zaidi.

"Matibabu ya watoto wadogo chini ya miaka mitano ni bure na huduma za mama na mtoto wa chini ya miaka mitano zinatolewa bila malipo yeyote," alisema Kiyenze.

Mganga wa zamu katika wodi namba sita ya watoto wachanga katika Hospitali ya Manispaa kahama, Philipo Laizer alisema walimpokea mtoto wa kiume mwenye uzito wa kilo tatu na nusu kutoka kituoni hapo. Alisema walipomfanyia uchunguzi waligundua amevunjika mkono wa kulia na kuufunga mkono nusu ili kuupa nguvu.

Aidha, baba wa mtoto huyo, Jumanne Paulo alithibitisha kurejeshewa fedha hizo baada ya kutoa taarifa kwa uongozi ngazi mbalimbali.

Jana, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha alimtembelea mtoto huyo hospitalini ili kumjulia hali na kuthibitisha kuwa suala la rushwa tayari lipo katika mamlaka husika ambayo ni Taasisi ya Kuzua na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Macha alisema: "Yaliyoonekana kwenye kituo hicho cha afya ni mazingira ya rushwa yanayoonekana kwenye maeneo mengine ya kutolea huduma, tutaendelea kupiga vita ili wananchi wapate huduma stahiki"




Waziri wa Madini, Antony Mavunde (kulia), akipata maelezo kuhusu Barrick inavyowezesha Watanzania kupitia uwekezaji wake kutoka kwa Meneja wa Barrick nchini, Melkiory Ngido (kushoto), alipotembea banda la maonesho la kampuni hiyo jana kwenye mkutano wa jukwaa la tatu la utekelezaji na ushirikishaji Watanzania katika sekta ya madini unaoendelea jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 69 mbaroni tuhuma kuhusika na uhalifu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watu 69 kwa tuhuma za makosa mbalimbali ikiwemo uhalifu katika maeneo tofauti ya Chuo cha Mtakatifu Agustino (SAUT).

Hatua hiyo inafuatiwa kuwepo kwa matukio mbalimbali ya uvamizi katika maeneo ya chuo hicho, ikiwa ni pamoja na kujeruhiwa kwa wanafunzi na wafanyabiashara kisha kunyang'anywa mali zao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, DCP Wilibroad Mutafungwa alithibitisha kukamatwa kwa watu hao jana na kusema walikamatwa katika operesheni ya siku tatu iliyofanyika katika Kata ya Luchelele jijini hapa.



DCP Mutafungwa alisema operesheni hiyo ilianza Mei 18, ilifanikiwa kukamatwa kwa watuhumiwa hao wakiwemo wanachuo wa chuoni hapo.

"Baadhi yao wamekamatwa na mali mbalimbali zinadhaniwa kuwa ni za wizi, matumizi ya dawa za kulevya, kucheza kamali pamoja na kujipatia kipato kwa njia ya ukahaba,"alisema DCP Mutafungwa.

Vilevile alisema katika operesheni hiyo zilikamatwa pia mali zinazodhaniwa kuwa za wizi ikiwemo televisheni pamoja na pikipiki nne.

Kamanda Mutafungwa, alisema uchunguzi bado unaendelea na watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani pindi utakapokamilika.

## Wakatishwa masomo kwa ujauzito

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WANAFUNZI wawili kutoka Kata ya Mwamala Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (majina yamehifadhiwa), wamekatishwa masomo baada ya kupata ujauzito katika umri mdogo.

Taarifa hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwamala, Suzana Kayage, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa mradi wa wanajamii na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na SPC kwa ufadhili wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Alisema mmoja wa wanafunzi hao alikuwa anasoma darasa la saba (14), aligundulika kuwa mjamzito Februari mwaka huu, huku mwingine (16) alikuwa akisoma kidato cha pili katika Shule ya Sekondari ya Kiselya ambaye tayari amejifungua na anaendelea na malezi ya mtoto.

Alisema baada ya tukio hilo walitoa taarifa kituo cha polisi kwa hatua zaidi za kisheria na kupewa namba SHI/RB/531/2024 kwa mwanafunzi wa darasa la saba ambaye alimtaja Dotto Ngassa (kaka yake wa ukoo) kuhusika na ujauzito huo kisha kutokomea kusikojulikana.

Alisema walikuwa wakikutana usiku kwenye mikesha ya harusi zinazofanyika kijijini akimlaghai kwa Sh.2,000 hadi Sh. 5,000 ambazo alikuwa akizitumia kwenye mahitaji ya shule.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata, Sophia Philbert alisema kwa kuona ukubwa wa tatizo hilo wameendelea kuwafikia wanafunzi, wazazi na walezi kuwapatia elimu ya ukatili wa kijinsia.

## Baba kortini tuhuma kufanya mapenzi na mtoto wake

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

MKAZI wa Nyakato mkoani Mwanza, Bashir Mohamed (35) amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya Ilemela kwa kosa la kufanya mapenzi na mtoto wake (jina limehifadhiwa).

Mohamed alipandishwa mahakamani hapo juzi na kusomewa shtaka katika kesi ya jinai namba 13448/2024 ambapo anadaiwa kulitenda kati ya Septemba mwaka jana hadi Februari 15 mwaka huu.

Akisoma shtaka hilo, Mwendesha Mashtaka wa serikali, Mwanahawa Changale, alisema mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo kwa nyakati tofauti kati ya Septemba, 2023 hadi Februari.

Aidha, alisema mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume na Kifungu Namba 158 (1) (a) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Aya ya 16 kilichofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, mshtakiwa alikana na kuomba kupewa dhamana akisema shtaka linalomkabili linadhaminika.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Mkazi Mwandamizi, Juma Opudo alimtaka mshtakiwa kuitimiza masharti ya dhamana ambayo ni kuwa na wadhamini wawili watakosaini hundi ya maneno ya Sh.milioni nne kila mmoja na mwingine awe na mali isiyohamishika.

Hata hivyo, mshtakiwa alishindwa kutimiza masharti hayo kwani barua ya udhamini ya mdhamini mmoja aliyetokea wilayani Magu haikuthibitishwa na Hakimu Mfawidhi wa wilaya yake.

ama
ALHAMISI MEI 23, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Pata undani wa uvuvi haramu unavyotesa uchumi buluu kustawi Afrika Mashariki**



**ISREY AYOUB**
**Binti mwenye kifafa aliyesomea udaktari, adumu kuwa balozi na fani tiba imwajiri**

Ukurasa 12

# Kilichojificha nyuma ya pazia Rais Dk. Samia 'kila kitu afya ni lazima'

**Na Mwandishi Wetu**

PENGINE inaweza kuhojiwa kwa kina, miongoni mwa maeneo yanajitafsiri katika uwekezaji wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni sekta afya na mahsusi akinoa na kuboresha ubunifu ulioasisiwa na viongozi watangulizi wake, anaunganisha na ubunifu wake.

Kwa nafasi ya pekee, nyenzo inayotumika kufanikisha miradi na mikakati hiyo kitaifa ni Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), uliopitishwa mwaka 2007 na kuanza kazi 2008, zama za serikali ya Awamu ya Nne. Dk. Samia akiwa katika Baraza la Mawaziri hilo.

Kama watafiti wanavyofafanua mara zote, chanzo cha kitu kisicho wazi sana, njia mojawapo ya kufahamu ni kufanyia kazi chimbuko lake au mzizi (etymology).

Moja kwa moja inaporejewa historia yake, mkuu huyo wa nchi awamu ya sita, ana unasaba wa moja kwa moja na maeneo makuu kadhaa, mbali na siasa.

Hayo ni; biashara, huduma za jamii, maendeleo ya kinamama na watoto hali kadhalika afya, ambayo ina undugu wa karibu na ustawi wa mama na watoto afya.

Hapo inayomuweka katika umahiri, uzoefu na utashi huo, kwamba anawafahamu vilivyo kinamama, watoto, pia huduma afya na mahsusi katika virusi vya Ukimwi.

Pia, ni hali inayofanya hata alipojikita katika mamlaka ya kisiasa, huwa habaki mbali na mambo hayo; leo akiwa mkuu wa nchi ni adimu sana kumkuta ziara na matendo yake yako mbali na sekta za afya, maendeleo ya watoto na



Rais Samia akizindua magari ya kubeba wagonjwa, katika hafla iliyofanyika, Dar es Salaam Oktoba, 2023. **PICHA: MTANDAO.**

ustawi wa jinsia yake, kinamama.

Maambukizi ya VVU yafikia 7.2 waathirika zaidi ni wanawake na wasichana. Sasa hata majirani, pia wenzake wanaoongoza mataifa kwingineko wanamjua katika hilo na wanataka kupata 'mawili matatu' kuhusu sekta ya afya.

Ni ushahidi unaoweza kuwekwa na matukio ya hivi karibuni katika ujio nchini wa Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamud, ambaye akatembelea kujifuza nchini, katika Bohari ya Dawa (MSD), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), pamoja na Taasisi ya Mifupa ya (MOI).

Jambo hilo likaonekana nchini, katika taarifa ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza (sasa Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi), Machi 2023, akitaja maeneo ya mafanikio kwao na taifa kwa jumla ni hatua ya rais huyo kukabili kupinga ukatili wa kijinsia kwenye maeneo yote na vita dhidi ya Ukimwi.

Katika tafsiri pana, ndio kitaifa kunaonekana mageuzi na ujenzi mkubwa katika hospitali, zahanati na vituo vya afya kitaifa, vifaa tiba, dawa na elimu kwa wataalamu.

Inapotajwa hoja kwa kielelezo; inayohusu, iko katika kilichorejewa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, wakati MSD ilipokabidhi dawa na vifaa tiba vya zaidi vya Sh. bilioni 1.61 kwa vituo vya afya na hospitali za wilaya hiyo.

Akasema, hatua hiyo ya Rais Dk.Samia kwa Mvomero ni funga kazi kwani hajawahi kutokea.

Mkuu wa Wilaya huyo akasema, hatua ya MSD kutoa dawa na vifaa tiba hivyo kwa mkopo, imeacha alama kwa wilaya hiyo, ikizingatiwa ni eneo la kiuchumi na hakuna utajiri wa hospitali nyingine za umma wilayani hapo.

Hapo, Meneja wa MSD Kanda ya Dar es Salaam, Betie Kaema, akawaunga mkono akitamka: "chini ya Rais Dk.Samia, tutarajie makubwa zaidi."

"Mpango mkakati uliopo ni kuona dawa na vifaa tiba vinakuwa vya kutosha na kuwapo na akiba katika hospitali na vituo vyetu vya kutolea huduma. Kwa sasa tumeanza kuleta vifaa vya afya mara sita kwa mwaka huku maboresho mengine yakiendelea."

Simulizi kama hiyo, ndio ikaanguka mkoani Dar es Salaam mwaka mmoja baadaye, Mkuu wa Mkoa, wa Dar es Salaam Albert Chalamila alipowakabidhi wabunge wa majimbo 10 ya mkoani kwake, vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 691 vilivyotolewa na serikali kwa majimbo hayo.

Hizo ni miongoni mwa vifaa vilivyozinduliwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kwa nchi nzima vikiwa na gharama ya Sh. bilioni 14.9 kwa majimbo na halmashauri 214 nchi nzima.

Mkuu wa Mkoa Chalamila, akasema Rais Dk. Samia amedhamiria kumaliza vifo vinavyosababishwa na uzazi, hivyo uwekezaji mkubwa unaendelea kufanyika katika sekta hiyo.

"Mbali na kupokea vifaa hivi, jiji hili limenufaika na uwekezaji huo mkubwa unaohusisha uboreshaji wa miundombinu, vifaa, utoaji huduma huku utekelezaji wa miradi mingine mipya ukiendelea," anasema.

Naibu Spika wa Bunge Mussa Zungu, naye akatolea ufafanuzi, akianza na kumpongeza Rais kutoa magari ya kubebea wagonjwa kwa wabunge wote 528, lengo likiwa kuboresha Sekta ya Afya nchini.

"Rais Dk. Samia mpaka Novemba mwaka 2023 peke yake amewekeza zaidi ya Sh. trilioni sita katika afya. Mwezi uliopita kila mbunge amekabidhiwa gari moja na wabunge wako 528 wamepatiwa gari la kubeba wagonjwa.

"Rais Samia ametoa magari hayo kwa wabunge kwa lengo likiwa kuhakikisha vifo vya mama na watoto vinapungua," akasema Naibu Spika Zungu, Mbunge wa Ilala.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, akatoa ufafanuzi kwamba, vifaa hivyo ni sehemu ya mkakati wa serikali kukabiliana na changamoto ya vifo vya mama na mtoto, akisema ni mkakati wa uliozinduliwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu

AFYA

ISREY AYOUB

# Binti mwenye kifafa aliyesomea udaktari, adumu kuwa balozi na fani tiba imwajiri

**Na Christina Mwakangale**

ISREY Ayoub (25) ni shujaa wa kifafa. Amefanya mitihani ya taifa mara mbili, kidato cha nne na cha sita akiwa na hali hiyo.

Mara kadhaa akiwa pekee yake shule ya bweni, alikuwa na hali ya kuogopa inayoitwa 'hallucination', hisia zilizomfanya akipita eneo tulivu ahisi kuna hatari imemzingira.

Isrey, alianza matibabu ya afya ya akili Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (sasa Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili) mwaka 2016, akiwa kidato cha nne, huku dalili hizo zikianza akiwa kidato cha kwanza.

Binti huyo mtoto wa mwisho kati ya watano, katika familia yao, ameielezea Nipashe katika mazungumzo maalum hivi karibuni, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dar es Salaam, katika kufahamu changamoto anazopitia pamoja na matarajio yake, takribani miaka minane tangu agundulike anaugua kifafa.

Yafuatayo ni mazungumzo yake, ya maswali na majibu na mwandishi wa makala hii:

**SWALI:** Jina lako ni nani na una umri wa miaka mingapi? Pia, unaweza kuelezeaje hali yako?

**JIBU:** Naitwa Isrey Ayoub. Mimi ni miongoni mwa wanaopata changamoto ya kifafa. Nina miaka 25.

Kwa takribani miaka sita sasa, hali imekuwa ikinipata rasmi nikiwa kidato cha nne. Nilikuwa nakutwa na degedege mara kwa mara, nilipokuwa kidato cha nne.

Baada ya hapo, sikufahamu nilikuwa naumwa nini. Nilikuwa nasoma shule ya bweni, hivyo mara nyingi nilikuwa narudi nyumbani, napatiwa dawa kama vile za kupaka.

Nilikuwa nikisali sana, nikitumia dawa za kujifukiza kutoka kwa waganga wa kienyeji. Lakini kulikuwa hakuna matokeo yoyote, nikamaliza kidato cha nne.

Shule ya sekondari nimesoma Kazima, ipo mkoani Tabora. Wazazi wangu walikuwa wanakaa Dodoma. Niliporudi, wazazi wakaniona kwa mara ya kwanza nikiumwa, kumbuka nilikuwa niko shule ya bweni, kwa hiyo kilichokuwa kinanisibu wazazi wangu walikuwa hawajui.

**SWALI:** Kwa mara ya kwanza wazazi wako walipogundua una tatizo hilo, nini kilitokea?

**JIBU:** Wazazi wangu mara ya kwanza, mama akaniona na baba, sijui walibaini nini. Nikaumwa mara tatu au mara nne nikawa naenda kwa kiongozi wa dini 'ustadhi' ananiombea, kwa kuamini kwamba ilikuwa ni mapepo, pepo wabaya.

Baada ya hapo, baba akasema ngoja twende Mirembe Hospitali (Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili) ... tumefika Mirembe, nikakutana na daktari. Ingawa kabla ya hapo



Isrey Ayoub

nilielezea historia yangu.

Nikiwa kidato cha kwanza, nilikuwa nakumbwa na 'hallucination' (woga na fikra zisizio sahihi kma harufu, kadhia au kuguswa, ikijenga woga).'

Nilikuwa nasoma kijijini (bweni), kulikuwa na miti, mibuyu. Nilipopita, nahisi kama nakumbwa na watu wa hatari, naogopa, hii hali wanaita 'hallucination'.

Unajihisi kama uko eneo tofauti na eneo halisi ulipo. Nahisi nimegubikwa na nguo nyingi. Nikaelezea hivyo kwa daktari. Yaani hata kulala peke yangu nilikuwa naogopa.

Nilikuwa nalala na mama, baba. Kwa hiyo nilivyokuwa Tabora nikizipata hisia hizo, naogopa 'nahisi anxiety (wasiwasi) napita pembeni kama nipo njiani.

Nakumbuka daktari akaandika 'epilepsy' (kifafa), nikajisemea ahaaa! Nikapewa dawa za vidonge za mwezi, ilikuwa mwaka 2016. Kwa mwezi mmoja nikazitumia.

Nikarudi mwezi mwingine tena kuchukua dawa. Matokeo ya kidato cha nne yalitoka. Kliniki yangu ya kwanza ilianzia Mirembe. Dawa natumia mara moja kwa siku, kila siku usiku, vidonge vinakuwa vinne, hadi sasa.

Kila siku natumia dawa, mimi ni msichana, ni binadamu! Kumbuka kuna muda mwingine ninasahau, nachoka kumeza. Nikaenda sekondari ya juu, Bwiru Girls, sio kama nilikuwa sipati hizo 'episode' (vipondi), za degedege nilikuwa napata.

Nilikuwa napata pengine kwa sababu ya uzembe, simezi dawa. Lakini, kumbuka mzazi yeyote huwa anatarajia na kufanya kila awezalo, ili mtoto wake apone.

Kwa hiyo, nikawa naendelea kujifukiza, nikawa napelekwa kwa waganga tofauti, ili hii hali iishe. Nibaki kuwa Isrey yule wa kwanza. Changamoto nyingi nilizipata shuleni, nikamaliza elimu sekondari ya juu.

**SWALI:** Ulipohitumu kidato cha sita ndoto zako au ulitarajia kujiunga na elimu ya juu?

JIBU: Nilipomaliza kidato cha sita, nikajiunga na St. David College Health & Allied Sciences, mwaka 2019, hapa Dar es Salaam.

**SWALI:** Kwanini uliamua kusoma eneo la afya?

JIBU: Nilikuwa na rafiki yangu, Prisca, wote tulipata 'division' ya tatu na yeye alikuwa amesomea PCB na mimi nilisoma CBG. Tukikaa dada yangu na yeye, akasema anakwenda kusomesha 'Clinical Officer', ikanishawishi.

Ingawa nilipenda kusomea 'Nutrition', ila yeye akaenda kusoma chuo kipo Iringa, mimi nikasalia hapa (Dar es Salaam) katika chuo nilichosoma. Nimesoma miaka mitatu, udaktari ngazi ya diploma.

**SWALI:** Unatarajia kuendelea na masomo hayo?

JIBU: Inshaalah! Natarajia kusoma zaidi miaka kama mitano hivi, ili niwe daktari kamili.

**SWALI:** Changamoto gani ambazo unapitia, hasa ukizingatia unameza dawa kila siku, jamii, watu wa karibu wanakuchukuliaje?

**JIBU:** Mara ya kwanza, kwa sababu nilijua naumwa...degedege, inapoanza kuja unahisi. Ukishakata mawasiliano ndio inakuwa hujui kinachoendelea. Ila mwanzo inapoanza, unajitahidi kuomba msaada...nisaidieeee nisaidieee...ila sauti haitoki.

Mpaka mwisho, unapoteza fahamu. Kwa hiyo kutumia dawa, nikawa sijali mtu, kwa sababu nilikuwa na bidii darasani, ila nilipoanza kuumwa nikawa nakaa nyumbani hata wiki tatu, hata mtihani wa 'mock' kidato cha sita sikufanya.

Nakumbuka niliendа hospitali, wakasema unameza vidonge vingapi? Nikasema vinne, wakaniongezea. Hivyo nikawa naumwa mwili unalegea. Nikaondoka Mwanza...dawa zilinifanya nilale sana hata darasani, nilikuwa naumwa sana kichwa.

Kwa sababu ukitokewa na hali hiyo, ukishapata fahamu, kichwa kinauma sana.

**SWALI:** Uliwahi kuambiwa sababu au chanzo ni nini?

**JIBU:** Dawa nameza, vipimo bado sijafanya...vipimo ni gharama, hadi uende ustawi ufanye utaratibu, upate kibali. Kwa kuwa nilikuwa nasoma sikupata muda wa kutosha kushughulikia kibali.

Dawa nanunua kwa fedha taslimu na kwa mwezi Sh. 10,000 inanitosha na hata mimi mwenyewe kwa fedha yangu nahakikisha sikosi 'phenobarbital' (dawa inayotumika kutibu au kuzuia kifafa) kwenye kabati.

**SWALI:** Ulitarajia kuwa nani tangu ukiwa mdogo?

**JIBU:** Mimi naitwa Daktari Isrey (kicheko)...ingawa nilipenda kuwa mwanamitindo, napenda sana na mtu akitokea akiwekeza kwangu, tutafanya kazi.

Kwa sasa natamani nipate kazi nzuri, ingawa pia napenda kujikita katika kutoa elimu, ushauri kuhusu kifafa. Kupaza sauti kwa kujiamini, natamani niwe daktari na nimiliki taasisi binafsi.

Kwenye akili yangu nawaza... nitengeneze kitu tofauti kwenye jamii, labda msichana mrembo mwenye 'epilepsy'. Napenda kupambania kizazi changu, ili aliyeko kuanzia 2020 ajue nini cha kufanya, watoe zile dhana hasi kwenye akili zao.

**SWALI:** Kuna tahadhari zozote huwa unachukua kwenye maisha yako?

JIBU: Mimi ni mtu ambaye kwanza natembea na dawa zangu, pia mimi kifafa huwa kinanikuta usiku, usingizini. Nikiwa nimelala nashtuka, zinaanza 'hallucination'.

Zamani, lakini hata sasa, mkono wa kulia unaanza, hapo nitakimbilia kufuata vidonge ili nimeze. Nainuka, najua kabisa hapa naumwa, lazima nitafutie dawa. Nikimeza ni ninakuwa kama natulia, ila bado nakutwa kama 'mawenge'.

Tahadhari nyingine, ni kwamba mama yangu ananiambia nisiende kuogelea. Lakini, kama nipo na rafiki zangu wanataka tukaogelee, sikatai, naenda. Pia, kupika napika. Kwa ufupi, mimi mchana niko vizuri, ila kifafa kinanikuta usiku nikiwa nimelala.

Mimi nimesoma na wanafunzi ambao mwingine unakuta kaanguka. Mwanafunzi unajua ni mbishi utakuta ana dawa, hamezi!

**SWALI:** Je, huwa unatoa elimu kwa jamii, kuhusu hali yako?

**JIBU:** Ndio. Nimekuwa balozi. Ila changamoto utakuta mtu anakufuata anasema ...'dada Isrey lini tutapona kabisa, tufanyaje ili tupone?'... Mi nawaambia tu, tutumie dawa vizuri. Ukiona dawa haikusaidii vizuri, rudi hospitali.

Napenda kusema, jamii iache unyanyapaa. Watu wanaachika kwenye ndoa, wanafukuzwa shule, au mtu anashindwa 'ku-date'na mtu, eti kwa sababu ana kifafa.

Kuna changamoto wazazi wanapitia, utakuta anaambiwa...' Sasa wewe ina nini mtoto wako mwenyewe ana kifafa...'

Mtaani unyanyapaa! Utakuta mtu anaanguka, watu wanashtuka, wanashangaa, wanaanza kupiga kelele, ukipata fahamu, unakuta watu wamejaa, wanahadithiana awali ilikuwaje unasikia yote.

Imewahi kunitokea mara mbili, mwenzangu akaenda kumuita mwenye nyumba. Nikashtuka watu wamenijalia. Kwenye kazi pia, huwezi kujitangaza una kifafa, huwezi kupata.

**BINGWA AFYA YA AKILI**

Mtaalamu Bingwa wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka MNH, Dk. Saidi Kuganda anasema wanaougua kifafa, rekodi ya muda wa kupoteza fahamu kwa wanaougua ugonjwa huo mara nyingi ni ule ule.

"Huishi kwa masharti fulani fulani, namna ya kulala, yaani ulale upande upi kitandani, hasa usiku, haulali tu ovyo, ulale ubavu, usilale kifudifudi wala chali.

"Ukiona ukilala ubavu ukajikuta umegeuka si kwa fahamu zako, basi weka utaratibu wa kuegesha mto upande mmoja, ili hata iweje ujikute upo upande uleule." anasema bingwa huyo, ambaye ni Makamu Mwenyekiti cha Chama cha Wataalamu wa Afya ya Akili (MEHATA).

Anasema ugonjwa huo, sababu ya kwamba ni wa kurithi ni ndogo sana, chanzo kikuu ikiwa ajali. Maambukizi kwa watoto wakiwa na umri wa chini ya miaka mitano.

Sio ugonjwa wa kuambukiza, akishauri bingwa huyo na kufanua kwamba, wagonjwa hao wakikumbwa na hali tofauti, wapewe msaada.

AFYA

MARY KIPINGILI

# ...Kijana Ofisa Tabibu mwenye kifafa, asimulia milima na mabonde tangu F4

**Na Romana Mallya**

WAKATI kuna simulizi za unyanyapaa kwa wenye kifafa, hata kuwakosesha fursa muhimu kijamii, ikiwamo elimu, Ofisa Tabibu, Mary Kipingili, mgonjwa wa kifafa, ana simulizi kuhusu milima na mabonde yanayowasibu.

Anasema, ni takriban miaka minane sasa tangu agundulike kuugua kifafa, wakati huo akisoma kidato cha nne.

Ilikuwaje? Mary anasimulia, mwaka 2016 akiwa mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Hekima, Dar es Salaam, ghafla alisikia dalili fulani na kudondoka.

Anasema wakati huo hakuwahi kupatwa na tatizo kama hilo, hivyo uongozi wa shule ulimpeleka hospitalini, kujua kinachomsumbua.

"Nilikuwa ninasoma shule ya bweni. Kitendo cha kudondoka, kilisababisha nipelekwe hospitalini. Ilikuwa ni kwa mara ya kwanza kupata hali kama hiyo ya kuanguka.

"Baada ya vipimo nikagundulika nina kifafa. Nilipatiwa dawa nikaenda nazo shuleni nikazitumia mwaka mzima hadi namaliza kidato cha nne.

"Nilipomaliza shule nikaja Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) nikafanyiwa vipimo, nikaonekana nipo sawa, nikaacha kutumia dawa."

Anasema, aliporudi shuleni kuendelea na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Bukoba, kutokana na kuacha dawa, akawa anapata tatizo hilo la kuanguka kila siku.




Mary Kipingili

### AFICHA TATIZO

Mary anasimulia, alibahatika kupata watu shuleni wasio wabaguzi na mara nyingi alipoanguka na kuzimia, alipozinduka alijikuta tayari amebebwa kutolewa darasani.

"Nikizinduka, wananiuliza kama nina maumivu au majeraha yoyote. Kama ikitokea sina uwezo wa kubeba ndoo ya maji, walinisaidia.

"Muda mwingine, tatizo hili lilikuwa likinitokea nikiwa nimelala. Katikati ya usingizi nikishtuka, watakuja watanizunguka kwa sababu walikuwa hawajui shida ni nini," anasimulia.

Mary anasema akiwa katika hiyo hali, baadhi ya wanafunzi wenzake walikuwa wakimshika mikono, wengine miguu na kusali kila mmoja kwa imani yake mpaka akipata nafuu wanamuacha analala.

Anasimulia alidumu na hali hiyo hadi alipomaliza kidato cha sita shuleni hapo, bila wenzake kujua kilichomsibu.

"Sikutaka wajue, nilihofu kunyanyapaliwa. Nilipomaliza kidato cha sita, mwaka 2023 nilijiunga chuo na kusomea diploma ya utabibu. Hapo katikati nilirudi tena kwa daktari na kupatiwa dawa.

"Miongoni mwa changamoto nilizokumbana nazo ni kupata madhara ya dawa nilizopewa, nikabadilishiwa dawa nyingine na kubadilishiwa hospitali, baada ya mikono kuanza kutetemeka.

"Kwa sasa kliniki yangu ninakwenda Hospitali ya Muhimbili- Mlongazira kila mwezi kuchukua dawa. Ninaendelea vizuri," anasema.

### KUHUSU KAZI

Mary, mhitimu wa chuo mwaka jana 2023 na hajaajiriwa, ana ushauri kwa wazazi na walezi wenye watoto wenye kifafa, badala ya kupata hofu, wawapeleke hospitalini au vituo vya afya, wapate matibabu sahihi, ili watimize ndoto zao.

"Wazungu wanasema, 'time is money' (akimaanisha muda ni mali), kadri unapomchelewesha hali huwa mbaya," anasema na kutafsiri:

"Lakini ukimwaisha, hali itaboreka na ataendelea na masomo na kutimiza ndoto zake za kusoma hadi chuo kikuu na wapo ambao ni wanataaluma wazuri tu, lakini kama watapewa matibabu sahihi."

Anaeleza matibabu ya kifafa yanachukua muda mrefu na siyo anachokiita "sikutaka dawa za siku tatu halafu mtu aambiwe amepona..."

Mary anaendelea: "(Kifafa) kinahitaji moyo, kuwa mvumilivu ili hali iwe sawa na kuendelea kuboresha maisha na taaluma yako na kukuza uchumi wako bila ya kuwa tegemezi."

Mtaalamu huyo wa afya sasa ana ushauri kwa jamii kutohusisha ugonjwa huo na ushirikina, hali inayokwamisha tiba yake, akiwa na malelezo:

"Ugonjwa huu upo katika makundi ya magonjwa yasiyoambukiza. Kuna baadhi ya watu wanapomwona mtu mwenye tatizo hili, wanahusisha na masuala ya ushirikina.

"Hawa ni wagonjwa na wanahitaji tiba sahihi hospitalini, ili wapate nafuu na kuendelea na maisha yao.Wapo wanaodhani kwamba ugonjwa huu huambukiza, si kweli!...," anafafanua.

### MATIBABU YAO

Mary anatumia taaluma yake kuchambua taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), kuwapo takribani watu milioni 50 duniani wanaosumbuliwa na kifafa, Afrika ina zaidi ya wagonjwa milioni 10; Tanzania ikikadiriwa kuwa na watu milioni moja.

Kwa ujumla duniani, takwimu zinasema: "Inakadiriwa kuwa watu milioni sita hubainika na hali hii kila mwaka."

### UNYANYAPAA

Mary anasema, bado nchini kuna shida ya unyanyapaa kwa wagonjwa wake, akisema bado uelewa wa jamii kuhusu kifafa bado ni mdogo, dhana inayokaribisha unyanyapaa na ubaguzi kwa wanaoishi na kifafa.

Anasema unyanyapaa na kubaguliwa, umechangia kukosa haki zao za msingi katika maisha yao ya kila siku na hivyo, kudhoofisha ubora wa maisha yao.

"Kumekuwa na visa mbalimbali vya watoto kufukuzwa shuleni au kutopelekwa shuleni kabisa, kutoajiriwa au kufukuzwa kazi, kuvunjika kwa uhusiano au ndoa pindi mtu unapogundulika kuwa na hali za kifafa, na hata kufanyiwa vitendo vya kikatili vinavyotokana na imani za kishirikina," alibainisha.

Mary anaeleza zao la vitendo, ni kuwaletea msongo wa mawazo watendwa. Inaripotiwa, watu watano kati ya 10 wanaoishi na hali kifafa, wanapata maradhi ya wasiwasi au sonona, ikitajwa inawaweka na hatari ya kufariki mapema mara tatu zaidi ya wasiougua.

Anasema, wengi wanaoishi na hali hizo katika vituo vya afya kupata tiba sahihi, hivyo kuchangia usugu au ukali wa tatizo na madhara mengine.

### KAMPENI YA ELIMU

"Tunaungana na serikali pamoja na taasisi zote za kijamii na za kitaaluma katika jitihada zao na kampeni za kuelimisha jamii kupata ufahamu sahihi kuhusu kifafa ili kutokomeza unyanyapaa," anasema Muuguzi Mary.

Anasema kupitia Taasisi ya Wazazi wa Watoto Wanaoishi na Kifafa, wamezindua kampeni ya kuhamasisha jamii kuhusu uelewa wa maradhi hayo.

Daktari Bingwa Mbobezi wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Said Kuganda, ambaye ni, Mwenyekiti wa taasisi hiyo, anasema inawalenga wanaoishi na hali ya kifafa.

Dk. Kuganda anaeleza idadi kubwa ya wagonjwa wa kifafa wanaohudhuria kliniki, imepungua kutokana na changamoto mbalimbali, ikiwamo kukosa huduma ya bima ya afya.

"Zamani tulikuwa na mfuko wetu maalum, tunatafuta wafadhili wanatuongezea fedha, kisha tunatafuta dawa kiasi, hivyo aliyekuwa akikwama tulikuwa tunampatia dawa.

"Ilipokuja bima ya afya, watoto wengi walijiunga huko. Kwa hiyo dawa za kawaida zikawa zinapatikana huko. Kasi ya mfuko wetu ikapungua kwa kuwa wengi walijiunga katika bima ya afya, wakawa wanapata huduma hata kwa watu wazima.

"Bahati mbaya bima ya watoto ikafutwa ili kuanzisha iliyo bora zaidi. Tangu ifutwe na inayoboreshwa bado haijaja, tumerudi kwenye changamoto, wazazi wengi wanalalamika, hawaji tena kwenye kliniki kwa kuwa kila wakija wanaambiwa wanunue dawa, bima haifanyi kazi tena.

"Tumebaki na hii changamoto ambayo kidogo tunasema tuongeze sauti ifike kwa jamii kujaribu kuangalia namna wanavyoweza kusaidia jambo hili," anasema.

Anakiri kufahamu serikali ina dhamira nzuri katika mabadiiliko hayo, akiwataka wananchi wafanye juhudi kuijulisha serikali kuhusu kuwapo wenye hali hiyo wasio na bima afya, hata kuchangia kupungua wanaohudhuria kliniki.

"Tunaamini kitakachokuja kitakuwa kizuri zaidi, lakini tunataka serikali ijue kuna watu wanashindwa kuja kupata huduma kwa sababu ya hizi changamoto," anasema.

Hata hivyo, mtaalamu huyo, kwamba kwa mwaka huu baadhi ya dawa nzuri mpya zimeanza kuingizwa katika kifurushi cha bima ya afya, changamoto iliyoko ni watu hawana kifurushi chenyewe cha bima.

"Watoto wengi wanachukua bima shuleni, kwa hiyo kwa watoto wa kifafa wanaougua sana huwa hawaendi shuleni. Asipoenda, anajikuta hapati huduma. Tunaposema kuondoa unyanyapaa ni kujaribu kusaidia katika haki zao za msingi," anasema.

Mtalamu huyo bingwa, anaiomba serikali kuliangalia suala hilo, akinena: "Wengi wamepungua na hatuwezi kusema kwa namba. Sababu zipo nyingi hii ni kutokana na swali lako mwandishi wa habari.

"Sababu nyingine ni unyanyapaa ambao kabla hawajapata tiba nzuri unakuta mganga wa kienyeji ameshamwambia (mzazi au mlezi) tiba ipo huku."

### PENYE WAGONJWA WENGI

"Kwa sasa ukitembelea Ifakara, mkoani Morogoro kwa sababu ya visababishi (vya ugonjwa) vipo vingi. Imegundulika watu wengi pale wameathirika tatizo la kifafa, wapo kwenye matibabu na utafiti unaendelea, lakini inaonyesha kuna tofauti na maeneo mengine.

"Ila kila maeneo Tanzania kuna watu wanaishi na hali ya kifafa. Mfano hapa (Tanzania) wanasema karibu katika watu 1,000 kati ya 20 mpaka 37 huwa na hiyo hali, lakini kwenye hayo maeneo ambayo hali hii inaonekana ni kubwa zaidi," anasema bingwa huyo.

Anafafanua, wamekuwa wakihamasisha wenye kifafa kuwa makini na kufuatilia dawa na matibabu kwa ujumla, kwa kuwa tiba inaopunguza athari zake.

Kuhusu kampeni waliozindua, mtalaam huyo anasema itafanyika kwa mwaka mzima na ifikapo mwezi Novemba mwaka huu, watakuwa na mdahalo wa kitaifa kuhusu kifafa na namna bora ya kuwasaidia wanaoishi nayo.

MAZINGIRA

# Pata undani wa uvuvi haramu unavyotesa uchumi buluu kustawi Afrika Mashariki

## • Simulizi; ikolojia inavyobomoka, uharamia baharini




Samaki wakikaushwa kwa jua kwenye eneo la mwaloni Kigoma, Tanzania, ikiwa ni sehemu ya uchumi wa buluu. **PICHA: UN.**

**Na Maina Muiruri**

KINYUME na sheria, huko nyuma kunatajwa hakukuripotiwa na hata kusimamiwa kwa usahihi (IUU), uvuvi unaweza kuwa msamiati unaoeleweka katika uchumi wa buluu, huku ikionekana tishio kubwa kwa meli na mifumo ya uwiano wa hali ya hewa, vilevile jamii ya ufukweni duniani.

Ndani ya Afrika Mashariki, kunatajwa hali imefika pagumu ikiaathiri maisha ya mamilioni ya watu, ikitishia ustahimilivu na maisha ya watu hao, hali kadhalika rasilimali za baharini.

Maji yanayofika hadi penye fukwe za mataifa Kenya, Tanzania, Somalia na Msumbiji, yana utajiri wa viumbe asilia mbalimbali na viasilia vya kiuchumi, ingawa kuna umakini dhidi ya suala la usalama wa uvuvi mahali hapo.

Kwa ujumla, shughuli za kuvua zinajumuisha mambo mengi, baadhi yakikinzana na sheria za kitaifa na hata kimataifa, zikigusa mambo kama ukiukwaji matumizi ya leseni sahihi.

Pia, kunatajwa kasoro za kutoripoti matendo majini kwa mamlaka sahihi za usimamizi, kukiwapo miongozo na kuvua kusikoruhusiwa, au katika misimu isiyo sahihi.

### USIMAMIZI DUNI

Afrika Mashariki, kunatajwa tatizo hilo lilifika pabaya katika ukanda wake wa pwani, huku kukiwapo uwezo mdogo wa kumudu kupahudumia, hata uvuvi huo ukashika kasi inavyotakiwa katika ukanda wote tajwa.

Nchi nyingi za Afrika Mashariki zinatajwa kujitahidi na rasilimali zake na uwezo mdogo wa kumudu uhalisia wa mfumo wa utawala wake, hata zinashindwa kumudu vilivyo, shughuli za uvuvi zilizoko ufukweni.

Kumekuwapo rushwa za nyumbani na ukanda wa kimataifa, unaoendeshwa na kuunda njama, huku kukikosekana ustamilivu unaochangia kasoro.

Vyakula vya Majini: Hitaji kubwa la vyakula vya majini, linajenga msukumo wa kimataifa, ukigusa hata majumbani kunakotumiwa vyakula na lishe za majini.

Jamii zimeelemea katika vyanzo vya vyakula vya majini, samaki kuwa vyakula na vyanzo vya kipato cha umma, ilhali katika soko la kimataifa, hususan mabara ya Asia na Ulaya, kunajengwa mazingira ya kutanua uvuvi haramu.

Vivutio kiuchumi: Faida itokanayo na aina hiyo ya uvuvi haramu, ikahamia kuwa mvuto kwa wavuvi majumbani.

Inatajwa kwamba, licha ya kuanzishwa juhudi za kikanda kukabili hali hiyo katika nchi za Afrika Mashariki, uhusiano na utahibiti unaotarajiwa bado unatajwa haujafikiwa.

Hali ya kuwapo tofauti katika sera za kitaifa, inayokwamisha kufikiwa hatua zinazohitajika, kudhibiti nyendo za uvuvi haramu katika maeneo tajwa husika.

Athari hasi katika uvuvi huo unatajwa kujumuisha kuharibiwa mazingira, kunakonendana na uvuvi unaopita kiwango kinachotakiwa, vilevile kuharibiwa akiba ya mazalia ya samaki.

Ni hali iliyoharibu mfumo wa ikolojia (ecosystems) na afya ya viumbe maji, vyote vikichangia uharibifu na kuacha hasara kwa nchi.

Matokeo ya uvuvi huo haramu kitaifa na kimataifa, sasa yanagusa moja kwa moja athari hizo za kiuchumi ndani ya Afrika Mashariki.

Sura ya pili ni kwamba, nyendo za uvuvi halali zinakabliana na changamoto ya ushindani haramu, hata kusababisha kushika kipato na fursa za ajira.

Nayo ni hali inayotajwa kuendana na serikali kupoteza kipato kitokanacho na kodi, pia ada mbalimbali ambazo ni msingi wa juhudi za maendeleo kitaifa.

Eneo lingine linalotajwa, ni panapoathirika usalama wa chakula, ikizingatiwa mlo wa samaki ni chanzo cha protini. Hivyo, inatajwa penye 'kudoda' bidhaa husika kunaendana na magumu ya soko lake.

Lingine tajwa, ni magumu ya kijamii, yanayohusiana na athari inayojumuisha, umaskini ambayo nayo inachangia watu kuhama makazi, hali kadhalika maisha ya umma kutikisika kwa jumla, kutokana na magumu hayo kiuchumi.

Kinachofanyiwa kazi kwa kina sasa ni kasoro ya uvuvi wa kihistoria na utamaduni watu wanarithishana, ikiwa inagusa vibaya uchumi wa umma.

### UHARAMIA BAHARINI

Taifa la Kenya linaelezwa kuchukua hatua katika kukabili magumu ya uvuvi haramu, ikiwamo kuanzisha ulinzi maeneo ya Pwani ya bahari, kukabili uvuvi haramu, huku kukiwapo ushirikiano maalum wa ukanda pwani, katika nyendo hizo.

Hata hivyo, kwani bado kunashuhudiwa nyendo zilizo kinyume kisheria na ukiukwaji mbalimbali, dhidi ya uvuvi sahihi, ukifanya zaidi katika maeneo ya mafichoni.

Inatajwa baadhi ya maeneo kama ukanda wa majini kuelekea Somalia, ambako kuna utajiri wa asili wa samaki, kuna vyombo vya majini vinafanya uvuvi haramu kwa wingi, baadhi vikitokea mataifa ya Asia.

Pia, katika maeneo ya Somalia, kutokuwapo serikali imara kwa miaka mingi, nako kunatajwa kuchangia uvuvi huo hata ikatawala katika eneo hilo.

Kwa Tanzania, kunatajwa mapugufu ya kukosekana rasilimali za kutosha kufanyia utafiti katika eneo hilo.

Hiyo, inatajwa kutoa mzizi wa kwa nafasi ya uvuvi haramu katika baadhi ya maeneo, kukitumika zana haramu nyavu zisizotakiwa, zinazochangia uharibifu wa kimazingira na viumbe tajwa kwa ujumla.

Wataalamu wa uchumi wa buluu, wanasisitiza kwamba taifa linaaswa lijengewe uwezo katika mambo kama ya kuwekeza teknolojia, nchi ipige hatua katika mafunzo, teknolojia, nguvu kazi na hata kupiga faini dhidi ya wanaokinzana na maboresho tajwa.

Hiyo inatajwa kuendana na jamii kutumikia maendeleo yao, ikijikita katika mbinu bora na za kisasa katika uvuvi, ikiwamo elimu ya kuachana na kasoro zilizoko kwenye uvuvi.

Lingine linatajwa ni kujumuisha mbinu za manejimenti na usimamizi wake moja kwa moja, kwa mbinu mbalimbali na maeneo tofauti.

Inaelezwa, katika mtazamo na mbinu ya kuifanya hiyo kuwa ya kimataifa, kunahitajika ushirikiano unaobeba staili za kupeana taarifa, kuungana katika maazimio na ujenzi wa mkakati ndani ya nchi za Afrika Mashariki.

Maeneo mengine yanayotajwa kufaa kusukuma mageuzi hayo tajwa, yanajumuisha kupitisha mipango ya pamoja inayowezesha samaki kuvuliwa kihalali, kukitajwa umuhimu wa mwamko wa watumiaji kutumia yaliyo muhimu na halali kutumika majini.

Wadau hao wa uchumi wa buluu, wanasema namna ya kukabili uvuvi haramu ni kubomoa mzizi wake ulioko, katika ngazi zote kama za utawala na soko bora, hadi nguzo ya uhusiano bora kimataifa.

Wahusika wanajumuisha hilo na uamuzi mbalimbali kwa nchi za Afrika Mashariki, ambazo zikatetea mazingira ya usalama wa maji, kuipatia jamii usalama maji ukanda wa pwani.

**Mwandishi ni mdau aliyezama katika maandiko ya uchumi wa buluu na ustawi wake.**



# Waziri: Urasimishaji makazi utaboreshwa

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa amesema zoezi la urasimishaji linaloendelea maeneo mbalimbali nchini litaboreshwa ili kuleta ufanisi.

Silaa aliyasema hayo juzi wakati wa semina kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii juu ya utekelezaji Mradi Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi nchini (LTIP) hadi kufikia Mei 15, 2024 iliyofanyika Ukumbi wa Samwel Sitta, bungeni, jijini Dodoma.

Alisema maboresho hayo ya urasimishaji yatawafanya wananchi kuelewa kuwa kuishi eneo rasmi kama vile la mita za mraba 750, kuna faida zaidi kulinganisha na kuishi eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 1,000 lisilo rasmi.

**Tunapopanga na kupima maeneo, mtu anapopata kiwanja chake basi ajue nina kiwanja eneo fulani lakini kuna maeneo ya umma ambayo yapo na wakati mimi ninapata kiwanja nimeyalipia.**

Aliwataka wananchi wanaorasimishiwa maeneo yao kutekeleza dhana ya kujitolea wakati wa zoezi hilo kwa kuwa ndiyo dhana ya ujamaa na falsafa ya Tanzania inayomfanya mwananchi kuelewa sehemu ya eneo lake imetolewa kwa ajili ya matumizi ya huduma kama vile barabara, makaburi na shule.

Alisema utekelezaji huo ukifanyika, uvamizi kwenye maeneo ya wazi unaofanyika hivi sasa kwenye maeneo mbalimbali utapungua.

"Tunapopanga na kupima maeneo, mtu anapopata kiwanja chake basi ajue nina kiwanja eneo fulani lakini kuna maeneo ya umma ambayo yapo na wakati mimi ninapata kiwanja nimeyalipia," alisema Silaa.

Kwa mujibu wa Waziri Silaa kuna maelekezo kwa maeneo yanapopangwa na kupimwa kwamba mtu anaponunua kiwanja chake cha makazi ajue hawezi kuishi peke yake na atakuwa amelipia pia maeneo ya huduma kama vile ya kuabudu na kuzika.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda aliwaeleza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa wizara imeendelea kutoa elimu hususan kwenye maeneo yanayomilikishwa kwa hati.

Alitolea mfano uwekaji mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji kuwa zoezi hilo limekuwa likihusisha wananchi wa maeneo husika huku akiweka wazi kuwa elimu imekuwa inatolewa kwa makundi mbalimbali ili kujua umuhimu na namna ya kutunza hati.

"Ushirikishwaji katika zoezi la mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji ni mkubwa sana maana wanaokwenda kusimama na zoezi ni wananchi wenyewe. Kwahiyo, utoaji elimu ni mkubwa na wananchi wanaelimishwa kwa makundi ili kuelewa hati inayokwenda kutolewa," alisema.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendesha semina ya siku moja kwa wajumbe wa kamati hiyo kwa lengo la kuelezea hatua zilizofikiwa kwenye Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi Tanzania (LTIP) hadi kufikia Mei 15, 2024.

Mradi huo unatekelezwa kupitia vipengele vinne ambavyo ni kuongeza usalama wa milki za ardhi, kuimarisha mifumo ya taarifa za ardhi (ILMIS), kujenga miundombinu ya ardhi pamoja na kusimamia mradi.

## Sekta binafsi yatakiwa kujenga viwanda bora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Zanzibar, Omar Said Shabaan, amewahimiza wadau wa sekta binafsi kujenga viwanda vinavyozalisha bidhaa zitakazokidhi vigezo vya soko la nje.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua wiki ya viwanda na biashara katika viwanja vya Bunge jijini hapa.

Waziri huyo alisema wakati serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuondoa changamoto zinazoathiri ukuaji wa sekta za viwanda na biashara wadau katika sekta hiyo wanapaswa kuchangia juhudi hizo.

Hivyo, aliwaasa wadau kuwekeza katika viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini ili kuongeza wigo wa soko la ndani na kuajiri vijana wa kitanzania.

Hata hivyo, aliwaomba wabunge kuwaelimisha wananchi kuweza kupenda na kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya hapa nchini.

"Wadau wote nawaasa kuwa serikali itaendeleza juhudi za kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji na ujenzi wa viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025," alisema.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe alisema maonyesho hayo ni sehemu ya kutoa elimu kuhusu wizara hiyo ili Watanzania wajue kazi zinazofanywa na wadau mbalimbali ikiwamo sekta binafsi.

Alisema lengo la wizara ni kuonyesha namna ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan anaimarisha demokrasia ya kiuchumi na mazingira ya uwekezaji yanayovutia wawekezaji kuja kuweza nchini.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan 'Zungu' (kushoto), akikata utepe kuzindua Katiba na Mpango Mkakati wa Umoja wa Vijana Wabunge Tanzania (TYPC), jijini Dodoma jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Umoja huo, Zainabu Katimba (wa pili kulia) na (kulia) ni Katibu wa Umoja huo, Ramadhani Ramadhani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yatoa siku 30 wamiliki viwanda vya chai kulipa madeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa mwezi mmoja kwa wamiliki wa viwanda vya chai nchini kulipa madeni wanayodaiwa na wakulima wadogo wa zao hilo.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alitoa agizo hilo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Chai Duniani.

"Hadi kufikia Juni 20 mwaka huu wamiliki wote wa viwanda wanaodaiwa na wakulima wadogo wa zao la chai wahakikishe wanalipa madeni hayo ili wakulima wetu wanufaike na kazi waliyofanya katika kipindi chote cha msimu,"alisema.

Aidha, Silinde alisema serikali imeweka mikakati ya kuongeza uzalishaji wa zao ilo kwa kufufua mashamba yaliyotelekezwa na kujenga viwanda saba vya kuchakata zao hilo vitakavyomilikiwa na wakulima wadogo.

Alisema mkakati mwingine wa serikali ni kuhakikisha inaweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya chai ili wakulima walime misimu yote.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Chai Tanzania, Rukia Mwango alisema serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha zao la chai linasimama.

Alizitaja hatua hizo ni kutoa fedha kwa ajili ya kujenga viwanda saba vitakavyomilikiwa na wakulima wadogo, kutoa fedha kwa ajili ya kufufua mashamba ya chai ambayo yametelekezwa kwa muda mrefu.

Pia, alitaja changamoto zinazokabili zao la chai kuwa ni propaganda za baadhi ya watu ambazo zimechangia kudhoofisha soko la ndani la bidhaa hiyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chai Tanzania, Mustapha Umande, alisema lengo la kuadhimisha siku hiyo ni kutambua mchango wake katika kukuza ajira na kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Alisema, serikali imeweka kipaumbele kuhakikisha sekta hiyo inakuwa kutokana na umuhimu wake hasa kiafya, kwamba husaidia kupungua athari za magonjwa ikiwamo kansa.





# Maofisa TASAF 'feki' wadaiwa kuwatoza fedha wananchi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

BAADHI ya wasimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ngazi ya jamii wa Kijiji cha Mbeya One kilichopo katika Kata ya Isongole Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wanadaiwa kuhujumu mpango huo kwa kuwatoza michango wanufaika kinyume na utaratibu.

Viongozi hao wanadaiwa kukusanya Sh. 5,000 kwa kila mnufaika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa madaraja kinyume na maelekezo ya matumizi ya ruzuku inayotolewa na serikali.

Wakizungumza na Nipashe kijijini hapo, baadhi ya wanufaika hao walisema viongozi hao wamekuwa wakiwatembelea majumbani na kuwatoza fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa daraja lililopo kijijini hapo, ambalo hata hivyo linajengwa kwa ufadhili wa TASAF.

Mmoja wa wanufaika hao, Martha Mbelenje ambaye ni mzee alisema viongozi hao walifika nyumbani kwake na kumtaka atoe Sh. 5000 na alipohoji ni kwa ajili ya nini alielezwa kwamba ni kwa ajili ya ujenzi wa daraja.

Alisema aliwajibu kwamba hana fedha hiyo na badala yake ana Sh. 3000 na hivyo akawaomba alipe hiyo na wakakubali kwa masharti kwamba Sh. 2000 iliyobaki angemalizia akiipata.

"Kwa sababu wajukuu zangu walikuwa hawapo niliona nitoe ili wakirudi kutoka shambani waje wanisaidie maana mimi fedha ninayopewa na TASAF ni kwa ajili ya kusomesha wajukuu, kununua chakula na kuwapeleka wajukuu zangu kliniki," alisema Martha.

Mjukuu wa bibi huyo alisema bibi yake amekuwa akipatiwa fedha hizo kwa ajili ya kuendesha maisha yake na wajukuu zake ambao anawalea na alishastaafu kushiriki shughuli za maendeleo.

Alisema siku bibi huyo alipotozwa fedha hizo alimkuta nyumbani akiwa ananung'unika na alipomhoji aliambiwa kwamba wasimamizi wa TASAF wamemtoza mchango wa daraja na ndipo akamshauri aende kwa Mwenyekiti wa Kijiji.

Baadhi ya wakazi wa kijiji hicho walisema waliwashangaa watu hao kuanza kukusanya fedha hizo kutokana na kwamba daraja walilokuwa wanasema wanataka kujenga linagharimiwa moja kwa moja na mpango wa TASAF.

Mmoja wa wananchi hao, Gabriel Dosert alisema wakati daraja hilo linaanza kujengwa hawajawahi kuambiwa kwamba wanufaika wa mpango huo ndiyo watachangia bali mradi unatekelezwa moja kwa moja na TASAF.

Mwenyekiti wa Dosert Melele alisema michango iliyokuwa inakusanywa ilikuwa siyo halali na baada ya kupata taarifa aliwabana vijana waliokuwa wanachangisha na aliwaamuru warudishe fedha hizo na wasirudie kuwachangisha wazee hao.

"Kuna kijana anaitwa Pascal Mwandemele huyu ndiye aliyepita na wenzake kwa wazee hawa akawachangisha michango, niliwataka warudishe fedha zote na wakazirudisha, nilibaini kuwa vijana hawa siyo waaminifu kwa sababu TASAF wanatuletea miradi mingi sana," alisema Melele.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Rungwe, Lydia Mwakatumbula alisema miradi yote inayotekelezwa na mpango huo haichangiwi na wananchi isipokuwa wanufaika wanapata fursa ya ajira katika miradi hiyo na wanapaswa kulipwa.

Alisema ipo miradi ambayo inatakiwa kuchangiwa na kwamba miradi hiyo ni ile inayokuwa imeibuliwa na wananchi wenyewe na kwamba mradi wa Daraja la Kijiji cha Mbeya One linatekelezwa na TASAF moja kwa moja na wananchi hawachangii.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zainab Abdallah, akizungumza baada ya kuzindua huduma ya mkoba ya madaktari bingwa wa Rais Samia Suluhu, itakayofanyika kwa siku nne katika Hospitali ya wilaya hiyo ya Samia Suluhu jana. Wengine ni Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Gerald Kazumba (kulia), Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Juma Mombokaleo (wa pili kulia) na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Mohamed Mfaki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Neema watumiaji Barabara Mbalizi-Mkwajuni

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI wanaotumia Barabara ya Mbalizi -Mkwajuni, wameanza kupata matumaini ya kupungua kwa gharama za usafiri baada ya serikali kutangaza kuijenga kwa kiwango cha lami.

Barabara hiyo (km 92) inaunganisha mikoa ya Mbeya na Songwe hasa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Songwe ambazo zina utajiri wa madini na mazao mbalimbali.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi hao walisema wamekuwa wakipata shida ya usafiri kutokana na magari yanayopita barabara hiyo kuwa machache.

Mmoja wa wananchi hao, Maria Soho alisema ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Galula alisema nauli wanayolipa kwenye mabasi yaliyopo ni Sh. 8,000 kutoka katika eneo lao mpaka Mbalizi.

Alisema endapo barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami kama ambavyo serikali inaeleza nauli inaweza kushuka mpaka Sh. 4,000 na kwamba hata idadi ya magari itaongezeka.

Yohana Emmanuel ambaye ni dereva wa mabasi yanayofanya safari kati ya Mbalizi na Mkwajuni alisema wamiliki wengi wa mabasi wanaogopa kupeleka mabasi mazuri kwenye barabara hiyo kwa sababu ya ubovu wa miundombinu.

Alisema kwenye baadhi ya maeneo ya barabara hiyo hakuna madaraja hali ambayo inasababisha kipindi cha mvua kukwama kwa saa kadhaa wakisubiri maji yapungue ndipo waendelee na safari.

# Wanafunzi wawasilisha kero lukuki kwa RC Mtaka

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Ugera na Luana katika Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe wameiomba serikali kuwatatulia baadhi ya kero zinazowakabili ikiwemo ukosefu wa maji na umeme.

Wamesema ukosefu wa huduma hizo unawakwamisha kusoma kwa uhuru.

Aidha, wamesema shule zao hazina mabweni na mabwalo kwa ajili ya kulia chakula na kufanyia mikutano na mitihani, hali ambayo inawakosesha pia uhuru wanapokuwa shuleni.

Hayo yaliibuka katika mikutano miwili tofauti ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka katika ziara ya kutembelea miradi mbalimbali wilayani Ludewa.

Wanafunzi hao walisema kwenye suala la ukosefu wa maji linasababisha kwenda umbali mrefu na hivyo kukosa vipindi.

"Shule yetu haina maji inatulazimu kutembea umbali mrefu kutafuta maji na wakati mwingine tunachelewa vipindi darasani," alisema Steward Nyavike mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Luana.

Maltina Mchilo mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ugara alisema tatizo la kukosekana kwa umeme linasababisha kushindwa kujisomea usiku.

"Tunaiomba serikali ituletee umeme kwa sababu tunashindwa kusoma masomo ya jioni na katika nyumba tunazokaa hakuna umeme," alisema Mchilo.

Revino Mchilo mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Luana aliiomba serikali kuwajengea bweni na bwalo la chakula.

"Tunaomba serikali itusaidie kutujengea bweni kwa sababu hivi sasa tumepanga mitaani, na wakati wa chakula mvua ikinyesha hakuna sehemu ya kulia chakula," alisema Mchilo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Njombe Anthony Mtaka aliwataka wazazi na walezi wilayani Ludewa kusimamia elimu ya watoto ili kuwa na kizazi chenye tija.

"Maana yangu ni kwamba tusomeshe watoto kwa sababu hawa watoto kesho watakuwa viongozi lakini uone dunia ilivyo ya ajabu, watoto waliomaliza darasa la saba mwaka jana aliyechukuwa pesa ya kuozesha mtoto wake hivi anaakili kweli? kila mzazi apate uchungu," alisema Mtaka.

Hata hivyo, alisisitiza kwamba serikali inaendelea kutatua changamoto zote zinazojitokeza kwenye sekta ya elimu ili kuhakikisha watoto wanapata elimu bora.



# Serikali: Teknolojia imesaidia upatikanaji wa haki nchini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman amesema teknolojia inachangia katika kurahisisha upatikanaji wa haki mahakamani.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali lililoulizwa na Mwakilishi Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah, aliyetaka kujua kwa kiasi gani teknolojia inachangia urahisi wa kupatikana haki katika mahakama.

Akijibu swali hilo, Haroun alisema teknolojia hiyo huongeza uwazi na uwajibikaji kwa taratibu zote za uendeshaji wa mashauri, hali ambayo inaondoa changamoto ya urasimu na upendeleo kwa mashauri yote.

**Teknolojia hiyo pia hupunguza uwepo wa ulazima kwa wadaiwa pamoja na watumiaji wengine kufika katika majengo ya mahakama jambo ambalo huondoa usumbufu na gharama zisizo na lazima.**

Alisema teknolojia huharakisha upatikanaji wa haki kwa kuweka kumbukumbu sahihi na upatikanaji wa nyaraka za mahakama muda wote zinapohitajika.


Aidha, alisema husaidia kupata takwimu za usahihi na uhakika za mashauri yote yanayofika mahakamani kwa wakati wowote zinapohitajika na hupunguza mrundikano wa mashauri usio wa lazima, kwa kutoa taarifa za mara kwa mara za mienendo ya mashauri ikiwa ni pamoja na ughairisho.

Waziri huyo alisema pia huongeza uwekezaji kwa kuwa na uhakika wa mfumo wa utoaji wa haki ulio salama na kupatikana kwa muda wote.

"Teknolojia hiyo pia hupunguza uwepo wa ulazima kwa wadaiwa pamoja na watumiaji wengine kufika katika majengo ya mahakama jambo ambalo huondoa usumbufu na gharama zisizo na lazima," alisema.

Hata hivyo, alisema hurahisisha upatikanaji wa mienendo ya kesi na hukumu kwa utaratibu wa kutumiwa baada ya kesi kumalizika na pia uwepo wa teknolojia unasaidia kesi kuendelea kusikilizwa na kupokelewa ushahidi hata kama upande unaohusika katika kesi na mashahidi wapo nje ya eneo iliyopo mahakamani.

Vilevile, alisema kupitia teknolojia huduma ya wito kwa wananchi inarahisishwa kwa matumizi ya simu za mkononi na barua pepe katika hatua za kubadilishana taarifa za mtu kuitwa mbele ya mahakama pamoja na kulinda faragha ya watu maalum kama vile kesi za watoto, udhalilishaji.



Waziri wa Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Shaaban (kulia) na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (wa pili kulia), wakimsikiliza Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Alban Kihulla, walipotembelea Maonyesho ya Wiki ya Viwanda, bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Vijana waonyeshwa fursa kuwa matajiri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Godfrey Eliyakim Mzava, amewataka vijana kushiriki katika kilimo cha vanilla na viungo, ili kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao.

Alitoa wito huo jana wakati wa ukaguzi wa mradi wa shamba la vanilla na viungo huko Donge Mbiji katika Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

Alisema zao hilo linathamani na tija kubwa, hivyo ni vyema kutumia fursa hiyo ili kujikomboa na kuepukana na tatizo la umasikini.

Mwakilishi wa Dongo, Dk. Khalid Salum Mohamed alisema shamba hilo linapokea watalii wengi kwa kufanya utafiti na kuwawezesha vijana kujiajiri kupitia kilimo hicho.

Dk. Khalid ambaye ni Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi alisema shamba hilo ni kielelezo cha kuimarisha bidhaa za utalii nchini na kuwapatia kipato wananchi wa Donge na maeneo jirani.

Aidha, alisema Mwenge wa Uhuru kufika katika jimbo hilo kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo limezidisha ari na hamasa kwa wananchi kushiriki katika harakati za maendeleo.

Akisoma risala, Khamis Dola Khamis, alisema shamba hilo lina ukubwa wa ekari 12 na linauwezo wa kuzalisha zaidi ya Sh. milioni 19 kwa kilo 65 kavu.

Alisema kuwa soko la kuuzia bidhaa hizo lipo na tayari, kampuni kutoka Ujerumani imekubali kununua bidhaa zao wanazozizalisha.

Alisema kuwa ushirika huo unapokea vijana kwa kuwapa taaluma ya kilimo cha vanilla, viungo na bidhaa mbalimbali ikiwemo tangawizi, mchaichai, karafuu na binzari.

Mradi huo umeazishwa mwaka 2017 na unathamani ya zaidi ya Sh. milioni 100 na upo katika maeneo mbalimbali kama vile Mangapwani, Chechele na Karange ndani ya jimbo hilo la Donge.

## ACT-Wazalendo yataja mikakati ya ukuzaji uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema hakuna nchi yoyote duniani inayoweza kupiga hatua za maendeleo ya kiuchumi na kuondoa umaskini kwa kutegemea hisani.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo jana alipozungumza na wafuasi wa chama hicho Kiwani Mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema jambo pekee la kusaidia kukuza uchumi na kuondoa umaskini katika nchi ni kuwepo rasilimali na viongozi imara wenye uwezo wa kujitoa na kujitolea katika kusimamia na kuzitumia ipasavyo rasilimali hizo kwa manufaa ya taifa lao.

Alisema kwamba Zanzibar ina rasilimali nyingi na iwapo kutakuwa na mipango mizuri na usimamizi bora wa viongozi wenye ujuzi na maarifa ya kutekeleza vyema mipango inayowekwa ni wazi Zanzibar itakuza uchumi wake.

Othman alisema kwamba hivi sasa hali ya umaskini Zanzibar inaendelea kudhoofisha hali za wananchi kiuchumi na kimaendeleo na kuifanya nchi na wananchi kuwa na maisha magumu.

Aidha, alisema kwamba jambo lingine ni kuwepo ujasiri wa viongozi chini ya misingi ya haki katika uendeshaji na usimamizi wa masuala mbali mbali ya nchi.

Othman alisema kwamba Wazanzibari hawapaswi kuonea aibu uzanzibari wao kwa kuwa hiyo ni haki yao na kwamba ni jambo la msingi kuhakikisha kwamba haki hiyo wanaipata bila kuwepo vipingamizi.

Akizungunzia suala la muungano alisema kwamba siyo jambo geni duniani, lakini kinachohitajika ni kuwepo muungano wa haki unaojali utaifa.

Kadhalika, alisema kwamba katika suala la kuondoa umaskini pia ni jukumu la serikali kuhakikisha kwamba inatengeneza fursa za kiuchumi kwa wananchi, ili kusaidia kuongeza kipato chao na kwamba mataifa mengi yamefanikiwa kutokana na utaratibu huo.

Kuhusu ardhi, alisema kwamba ni miongoni mwa rasilimali muhimu ambazo wananchi wanaweza kufaidika kwa kukodisha kwa wewekezaji mbalimbali.

Katika ziara hiyo, Othman alifika Kijiji cha Mwambe Wilaya ya Mkoani kutoa pole na kuzifariji familia za ndugu Khamis Zahoro Makame, Othman Hassan Othman na Hashim Faki Makame waliofariki dunia baada ya kuzama baharini mkoani Mtwara wakiwa katika shughuli za uvuvi.

**Jambo lingine ni kuwepo ujasiri wa viongozi chini ya misingi ya haki katika uendeshaji na usimamizi wa masuala mbali mbali ya nchi.**



Mbunge wa Viti Maalum kwa wenye Ulemavu, Stella Ikupa akiuliza swali Bungeni jijini Dodoma jana, kuhusu serikali imefikia hatua gani kutoa mikopo ya elimu ya juu na kati kama ruzuku kwa watu wenye ulemavu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kanuni rufani ununuzi wa umma zaiva

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imepanga kuanza kutumia Kanuni za Rufani za Ununuzi wa Umma Julai Mosi, mwaka huu.

Aidha, mamlaka itatumia mfumo wa kuwasilisha malalamiko na rufani zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma lengo likiwa ni kuboresha eneo hilo.

Katibu Mtendaji wa PPAA, James Sando, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati wa kikao kazi cha kupokea maoni ya uandaaji wa Kanuni za Rufani za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 katika utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023.

Sando alisema Sheria Na.10 ya Ununuzi wa Umma ilitungwa na kupitishwa na bunge Septemba, 2023 na kwamba ili itumike vizuri, inategemea kanuni za ununuzi ambazo ziko katika hatua mbalimbali na zitakamilika na kuanza kutumika rasmi mwaka ujao wa fedha.

"Sheria iko tayari lakini haiwezi kutumika bila kuwa na kanuni ndiyo maana tupo hapa kwa ajili ya kupokea maoni ya wadau wa ununuzi kuhusu Kanuni za Rufani za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 ili kuiwezesha Sheria ya Ununuzi Umma ya Mwaka 2023," alisema Sando.

Aliongeza kuwa anaamini sheria hizo, zitapunguza changamoto kwenye rufani za ununuzi zilizokuwapo awali ambazo zilikuwa zinalalamikiwa na wazabuni.

Alisema baada ya kikao kazi kilichowakutanisha wadau wa ununuzi kutoka taasisi za umma, PPAA itaandaa kikao kingine na wazabuni ili nao watoe maoni yao kuhusu Kanuni za Rufani za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 kabla ya sheria hiyo kuanza kutumika rasmi.

Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma kutoka Wizara ya Fedha, Dk. Frederick Mwakibinga, ambaye alimwakilisha Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo, alisema serikali imefanya maboresho makubwa katika sheria hizo, hivyo watu watarajie mageuzi makubwa.

Dk. Mwakibinga alisema baada ya kanuni kukamilika, zitasaidia wananchi hususani wazabuni na wadau wa ununuzi kwenda kutumia kanuni ambazo zimekamilika na kuboreshwa na kuisaidia serikali kupata thamani halisi ya fedha katika miradi mbalimbali.

Alisema Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya mwaka 2023 imeboresha masuala mbalimbali ikiwamo kupunguzwa kwa muda wa kushughulikia malalamiko na rufani zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

# Chalamila atangaza kiama wakwepaji kodi

**Na Restuta James**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila ametangaza kuanza operesheni ya kubaini wakwepaji kodi na kutoa rai kwa wafanyabiashara kutoa ushirikiano ili jukumu hilo lifanyike kwa urahisi.

Pia ameonya wafanyabiashara kutoingia kwenye mgomo kuzuia zoezi hilo. Kufanya hivyo ni kukiuka 4R za Rais Samia Suluhu Hassan za maridhiano, kujenga upya, kuvumiliana na kustahimiliana.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Chalamila alisema lengo la operesheni hiyo ni kuhakiki matumizi sahihi ya mashine za kutoa risiti (EFD) kwenye maduka na maghala na stempu za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwenye vinywaji vikali na baridi.

"Kuna kasumba ya kuingiza vinywaji ambavyo havijathibitishwa na mamlaka husika kama ya viwango (TBS) na mamlaka zingine na hata zile zilizozalishwa hapa nchini, zipo ambazo zinauzwa bila stempu za TRA...Huu ni uhujumu wa uchumi wa taifa letu na uhujumu wa afya za Watanzania.

Mchakato tulionao hivi sasa ni kuendeleza operesheni kubwa ili kuwabaini wale wote wanaofanyakazi hizi kwa kuwa lengo lao ni kuhujumu uchumi wa nchi yetu.

"Mara kadhaa tumekuwa tukisikia harufu ya migomo kwa baadhi ya wafanyabiashara na migomo hii huja tu mara TRA inapotaka kuanza kufanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria katika maghala, maduka au operesheni za kuangalia matumizi sahihi ya EFD.

"Wafanyabiashara wowote watakaoinuka na kuanza kutangaza migomo hii, kwetu kama serikali migomo ni tamko la vita, nitoe rai kwamba Tanzania si nchi ya kivita Tanzania ni nchi iliyosimamia misingi ya maridhiano, kujenga upya taifa letu lakini zaidi kuvumiliana na kustahimiliana," alisema Chalamila.

Chalamila alielekeza wafanyabiashara wote wa vinywaji baridi na vikali kuhakikisha vinakuwa na stempu halisi za TRA, ili kodi iliyokusudiwa iweze kukusanywa.

"Serikali ipo tayari kuendelea kupokea maoni, kusikiliza na kufanya mabadiliko ya kisheria pale itakapolazimika kufanya hivyo," alisema Chalamila.

Aliieleka TRA kuhakikisha inawasaidia wafanyabiashara ili waweze kufanya kazi zao bila vikwazo vya kikodi.

Wakati huo huo, Chalamila amewataka wafanyabiashara na wakuu wa taasisi mbalimbali kufanya marejesho ya kodi kwa mujibu wa sheria kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

"Mfanyabiashara ni wakala tu wa kukusanya kodi kutoka kwa mwananchi kwenda serikalini, fedha hii inaenda kutoa huduma kwa wananchi. Tunapoelekea mwishoni mwa mwaka wa fedha, tufunge tukiwa tumelipa kodi vizuri ili tuijenge nchi yetu," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
23 - 05 - 2024

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya **tarehe 28-05-2024** hadi **03-06-2024** kampuni ya **FM CARGO LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAM** kwenda **TUNDUMA**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T611EDA/T682EAR**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 22 Upana - mita 4.30 Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **DSM, PWANI, MOROGORO, IRINGA, MBEYA, TUNDUMA** (Kuanzia saa **12:30 Asubuhi** mpaka saa **12:00 Jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**



KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KENEDY OKOTH NGUKA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Lexus yenye namba za Usajili **T400 CJF,** Engine No **IMZI543428,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/SHI/KAH/3405/2024**



KUPOTEA KWA CHETI



**DAUD JAPHET MATHAYO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2640.0031** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya JORMA mwaka 2012,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **PHQ/TAN/TAN/4515/2024**



KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MALUGU UMALA MAFANYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC148DMC** aina ya **HAOJUE,** rangi nyeusi, Chassis No, **1C6PCSKZNOA1600Z,** Engine No. **156FM13AD3F4S627.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DOD/BAHI/17961/2024**



KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUKALAI OMARI MTANGAZA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye usajili namba **T 582 CLR,** CHASSIS NAMBA: **NCP600192876** na ENGINE NAMBA: **2NZ3421574.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI NAMBA:
**PHQ/DAR/KIN/94322/2024**



KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RAMADHANI .M. BARAKA RASHIDI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za Usajili **MC 161 DDX aina ya HAOJUE** yenye Chassis **No,LC6PCJK29MOA 77961.** Engine NO:**156 PM 15 AD3F23095.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi:
Taarifa ya Polisi
**PHQ/RUV/SON/2409/2024.**



KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **TULA GEORGE KATINDASA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAUM** yenye namba za usajili **T673 DMP,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**PHQ/DAR/KIN/94750/2024**

## HABARI KIMATAIFA

# Israel yavamia kambi Jabalia yasambaratisha kwa mabomu

**GAZA, Palestina**

VIKOSI vya Israel vimejipenyeza ndani ya kambi ya wakimbizi ya Jabalia kaskazini mwa Ukanda wa Gaza na kufanya mashambulizi kwa kutumia ndege za kivita na vifaru.

Katika kambi hiyo jeshi lilitumia matingatinga kuyasambaratisha maduka na majengo mengine yaliyokuwa karibu na soko.

Jeshi la Israel lilidai kuwa limerudi kwenye kambi hiyo ambako miezi miwili iliyopita ilidai ilisema ililisambaratisha kundi la Hamas.

Wizara ya afya ya Palestina iliripoti kuwa vikosi vya Israel vimewauwa Wapalestina saba baada ya kuuvamia mji wa Jenin ulioko katika Ukingo wa magharibi.

Watu hao wameuwawa baada ya jeshi la Israel kufanya mashambulizi ya anga yaliyolenga maeneo 70 ndani ya saa 24 katika Ukanda wa Gaza.

Wizara hiyo ilisema watu wengine tisa wamejeruhiwa katika eneo la Ramallah na miongoni mwao, wawili wana hali mbaya.

Awali jeshi hilo liltangaza kuwa limeanzisha operesheni ya kupambana na ugaidi mjini Jenin.

Shirika rasmi la habari la Palestina (Wafa), liliripoti kuwa miongoni wa waliouwawa ni daktari bingwa wa upasuaji Usaeed Jabareen, wa hospitali ya serikali ya mjini Jenin. Limewataja watu wengine waliouawa ni mwanafunzi mmoja na mwalimu wake.

Wakati huohuo, Msemaji wa Wizara ya Kigeni ya Qatar, Hayo yakijiri, Majed Al-Ansari, amesema kuwa mazungumzo ya kusitisha vita Ukanda wa Gaza na kuwaachilia mateka kati ya Israel na kundi la Hamas yanaelekea kukwama.

Katika tukio linguine, nchi za Norway, Ireland na Uhispania zimeitambua Palestina kama nchi kamili, hatua ambayo imejulikana kuwa ya kihistoria iliyochukuliwa na nchi tatu za Ulaya. Waziri Mkuu wa Norway Jonas Gahr Stoere alisema hakuwezi kuwa na amani Mashariki ya Kati bila kuwepo suluhu ya madola mawili

Ireland nayo kupitia Waziri wake Mkuu Simon Harris imesema imechukua hatua hiyo iliyoitaja ya kihistoria kwa nchi yake na watu wa Palestina, kama njia ya kusaidia kupata suluhu katika mzozo wa Israel na Hamas ulioanza Oktoba 7, mwaka jana.

Wakati huo huo waziri wa mambo ya nchi za nje wa Israel Israel Katz, ameamuru mabalozi wa Ireland na Norway kurejea nyumbani mara moja kufuatia mataifa hayo kuitambua Palestina kama dola huru.

Kiongozi wa Palestina Mahmood Abbas amekaribisha uamuzi huo na kuyataka mataifa mengine kuchukua hatua kama hiyo.

*DW*



Gari lilobeba jeneza la aliyekuwa rais wa Iran, Ebrahim Raisi na viongozi wengine likipita mbele ya umati wa watu kwa ajili ya kuaga katikati ya jiji la Tehran jana. **PICHA: REUTERS**

# Wakenya waja juu bl. 3.9 kukodisha ndege ya rais

**NAIROBI, Kenya**

RAIA wa Kenya wameijia juu serikali yao kwa kufuja fedha za umma kwa kukodi ndege ya kifahari kwa ajili ya kumbeba Rais William Ruto, aliye nchini Marekani kwa ziara ya kiserikali.

Taarifa za gharama ya kukodi ndege hiyo ambayo serikali haijathitisha zilizotolewa na kituo cha televisheni cha KTN, inaeleza fedha zilizotumika kukodi ndege hiyo ni dola milioni 1.5 sawa na shilingi ya Tanzania, Bil. 3.9.

Hata hivyo, Msemaji wa serikali, Isaac Mwaura, alisema faida ya ziara hiyo ya Rais Ruto, hailingani kwa faida kubwa na fedha zilizotumika.

"Faida za ziara hii ni kubwa kuliko mara milioni pesa kama hizo," alisema Mwaura aliambia BBC, bila kuthibitisha gharama.

Katika ziara hiyo, kiongozi huyo ameambatana na ujumbe wa watu 30 akiwemo msanii wa vichekesho maarufu.

Rais Ruto na ujumbe wake waliwasiri jiji la Atlanta,katika jimbo la Georgia Jumatatu.

Kiongozi huyo yuko katika ziara ya siku nne kwa mwaliko wa Rais wa Marekani Joe Biden.

Ziara hiyo ni ya kwanza kwa kiongozi huyo wa Kenya kufanya nchini Marekani katika miongo miwili na ya kwanza kwa kiongozi wa Afrika katika kipindi cha miaka 16.

Akiwa nchini humo anatazamiwa kufanya mazungumzo na mwenyeji wake Rais Biden leo, ambayo yatalenga ushirikiano wa kibiashara na usalama, ikiwa ni pamoja na ahadi ya Kenya kuongoza ujumbe wa mataifa mbalimbali kurejesha hali ya utulivu nchini Haiti.

Hata hivyo, baadhi ya raia wa Kenya wameonekana kughadhabishwa na hatua ya kukodi ndege kutoka kampuni ya RoyalJet yenye makazi yake Dubai kwa ajili ya safari hiyo, badala ya kutumia ndege yake ya rais kwa ajili ya kubana matumizi ya serikali.

Hakuna maelezo yoyote kutoka serikalini kwa nini rais huyo alichagua ndege hiyo ya kibinafsi.

Hata hivyo, kumekuwa na wasiwasi wa usalama wa ndege ya rais, inayojulikana kama Harambee One, ambayo ilinunuliwa miaka 30 iliyopita.

Serikali ya Marekani ilikanusha ripoti kwamba ililipia ndege hiyo iliyotumiwa na Rais Ruto na ujumbe wake.

"Marekani haikulipia ndege ya Rais Ruto kwenda Marekani," ilisema ubalozi wa Marekani nchini Kenya.

# Ayatullah Khamenei aongoza kuaga mwili wa hayati Raisi

**TEHRAN, Iran**

IBADA ya mazishi ya aliyekuwa rais wa Iran, Ebrahim Raisi, zilifanyika jana katika jiji la Tehran na kuongozwa na kiongozi mkuu wa wa nchi hiyo, Ayatullah ali Khamenei.

Raisin, Waziri wa Mambo ya Nje, Hossein Amir-Abdollahian na maofisa wengine wa ngazi za juu waliofariki katika ajali ya helikopta iliyotokea Jumapili karibu na mpaka wa Azerbaijan.

Ibada hiyo ya mazishi ilifanyika katika eneo la Chuo Kikuu cha Tehran.

Serikali ilionya maandamano dhidi ya mazishi hayo na ujumbe wa matusi mtandaoni unaowalenga marehemu hao.

„Ee Mwenyezi Mungu, hatukuona chochote isipokuwa kheri kutoka kwake," Ayatollah Khamenei alisema katika swala ya marehemu kwa lugha ya Kiarabu.

Wakati wa ibada hiyo kaimu rais wa Iran, Mohammad Mokhber, alisimama karibu na jeneza na alionekana akilia hadharani.

Baada ya ibada hiyo wanajeshi walibeba jeneza kwenye mabega yao, huku kupiga kelele za kuipinga Marekani zilisikika kutoka kwa waombolezaji.

Majeneza yote walipakia kwenye trela na kuendeshwa hadi katikati ya jiji la Tehran katika uwanja wa Azadi Square, ambako hayati rais Raisi alitoa hotuba siku za nyuma.

Waliohudhuria walikuwa viongozi wakuu wa Jeshi la Ulinzi wa Mapinduzi la Iran, moja ya asasi yenye nguvu nchini.

Awali, umati mkubwa wa watu ulianza kukusanyika katika mji mkuu wa Iran Tehran kwa ajili ya sherehe za mazishi ya marehemu Rais wa nchi hiyo.

*BBC*



Wachezaji wa Tembo Warriors wakishangilia baada ya timu yao kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AAFCON), yanayoendelea nchini Misri. PICHA: MTANDAO




# TEMBO WARRIORS, GHANA MECHI MUHIMU AAFCON

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Walemavu (Tembo Warriors), inatarajia kukutana na Ghana katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Fainali ya Kombe la Mataifa Afrika (AAFCON), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa PetroSport ulioko Misri.

Tembo Warriors imemaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi D baada ya kufungwa mabao 2-1 na vinara wa kundi hilo, Angola katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi iliyochezwa juzi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Tembo Warriors, Salvatory Edward, alisema wameteleza kwa kufanya makosa na kuadhibiwa na Angola katika mechi hiyo ya pili.

Edward alisema tayari wamesahau matokeo hayo na wamejipanga vizuri kwa ajili ya mechi ya leo ambayo wanaamini watarekebisha makosa yao na hatimaye kupata matokeo chanya.

Kocha huyo alisema amewaona Ghana wanavyocheza na amejiandaa kukutana na mchezo wenye ushindani kutokana na ubora wa timu zote mbili zitakazokutana.

"Ninaimani kubwa na vijana wangu, wapo tayari kwa ajili ya kutafuta ushindi ili kupata nafasi ya kusonga mbele katika mashindano haya, benchi l ufundi tumemaliza majukumu yetu. kazi iliyopo kwa wachezaji lakini nawaomba Watanzania kuendeleza dua kwa ajili ya timu yao.

Kila timu itashuka uwanjani kwa lengo la kusaka ushindi, najua mechi yetu ya kesho (leo) tunatakiwa kupata matokeo bora ili kutuweka rekodi," alisema kocha huyo. Aliongeza malengo yao ni kufanya vizuri na kupata tikeyi ya kuiwakilisha Afrika kwennye Fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwaka 2026.

"Tutakuwa makini kwa sababu kila hatua tunayocheza ni ngumu, lazima tucheze kwa tahadhari katika michezo iliyopo mbele yetu hadi tutakapofikia kile tulichotarajia," Edward aliongeza.

Naye Mkuu wa Msafara Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Suleiman Selela, amewataka wachezaji kutokuwa wanyonge bali waendelee kupambana ili kuhakikisha wanatinga hatua ya fainali.

KANDANDA

## NEW CITY YAZINDUKA ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya New City FC imerejesha matumaini ya kubakia katika Ligi Kuu Zanzibar baada ya kuichapa Ngome mabao 2-0 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi.

New City sasa imefikisha pointi 30 na kupanda hadi katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo na kuwafanya mashabiki wao kuondoka na furaha.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Msaidizi wa New City, Razak Salum, alisema ingawa wamefanikiwa kujiondoa katika mstari wa hatari wa kushuka daraja lakini bado wanahitaji kupata ushindi wa michezo mitatu iliyobakia.

Salum alisema kufanya vyema katika michezo iliyobakia kutawasaidia kujiondoa kwenye hatari ya kushuka daraja kwa asilimia 100.

"Mafanikio tuliyoyapata ya kushinda michezo mitatu mfululizo yametokana na jitihada kubwa zilizoonyeshwa na wachezaji ambao hawakuvunjika tamaa licha ya kuwa na msimu mbaya. Jitihada hizi zinaendelea katika kuhakikisha hamasa kwa michezo mingine iliyobakia inakuwepo ili kufanikiwa kutimiza malengo," alisema kocha huyo.

Aliongeza kwa sasa kilichobaki ni kuhakikisha mashabiki wanakuwa sehemu ya kufanikisha ushindi.

## Ligi ya Wanawake kurejea tena Juni 7

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania inatarajiwa kurejea ifikapo Juni 7, mwaka huu baada ya kusimama kwa muda mfupi ili kupisha mashindano ya Shule ya Afrika yanayoendelea Visiwani Zanzibar.

Simba yenye pointi 43 ndio vinara wa ligi hiyo na anahitaji pointi moja katika mechi zake tatu zilizobakia ili kuwavua ubingwa JKT Queens yenye pointi 34, ikifuatia katika msimamo.

Vinara hao wamebakiza mechi ya ugenini dhidi ya Alliance Girls na baada ya hayo itarejea Dar es Salaam kuwasubiri Fountain Gate Princess na Geita Gold FC huku JKT Queens wakikabiliwa na michezo dhidi ya Fountain Gate Princess,Baobab Queens na Ceasiaa Queens.

Nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Ceasiaa Queens yenye pointi 29, watacheza mechi mbili ugenini dhidi ya Baobab Queens na Alliance Girls na itamaliza ligi nyumbani dhidi ya JKT Queens.

## Nasra, Najma kamili kuonyeshana ubabe

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa, Nasra Msami, amesema anatarajia kumchapa mpinzani wake, Najma Isike, katika pambano lao la Dar Boxing Derby litakalofanyika Juni 29, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Nasra alisema amejiandaa vyema kumkabili mpinzani wake ambaye 'hamuumizi kichwa' na anaamini atamaliza pambalo hilo katika raundi ya kwanza.

"Nimejipanga vizuri sana kuelekea katika pambano hilo, nimefanya maandalizi sahihi na ninaamini nitawapa burudani mashabiki wangu," alisema Msami.

Bondia huyo aliongeza amemfuatilia kwa karibu mpinzani wake na amejua madhaifu na ubora wake, na kwa sababu hiyo hana hofu yoyote kuelekea pambano hilo.

"Mimi huwa sipendi kuzungumza bali nitaonyesha kiwango changu wakati nitakapokuwa ninapigana, nimejiandaa kuonyesha vitendo, najiamini mimi ni bondia bora, " alisema Isike.

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO SOKONI ULAYA

MAURICIO Pochettino yuko katika rada ya Manchester United na Bayern Munich kama atondoka Chelsea kwa "makubaliano ya pande zote".***(Standard),***

### CHELSEA YASAKA KOCHA

KOCHA wa Stuttgart, Sebastian Hoeness na Kieran McKenna wa Ipswich Town wametajwa na Chelsea kama wanaoweza kuchukua nafasi itakayoachwa na Mauricio Pochettino.***(Teamtalk)***

### MARESCA ATAJWA CHELSEA

KOCHA wa Girona, Michel na Enzo Maresca wa Leicester City pia huenda wakawa miongoni mwa majina yanayozingatiwa na Chelsea. ***(Daily Telegraph)***

### TUCHEL KUREJEA ENGLAND

THOMAS Tuchel amefanya mazungumzo na Chelsea kuhusu kurejea katika klabu hiyo kwa kipindi cha pili. ***(Florian Plettenberg)***

### EDERSON, CITY KITAELEWEKA

KLABU ya Manchester City iko tayari kutoa ofa kwa mlinda lango wa Brazil Ederson mwenye umri wa miaka 30, ambaye anavutiwa na Saudi Arabia. ***(Fabrizio Romano)***

### GUEHI AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United inachunguza uwezekano wa kumsajili mlinzi wa Crystal Palace na England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 23, ikiwa watashindwa kufikia makubaliano na Everton kumnunua beki wa kati wa England, Jarrad Branthwaite (21). ***(Mail)***

### UNITED BAJETI KUBWA

MANCHESTER United ipo katika nafasi ya kutumia fedha nyingi katika dirisha la usajili la majira ya joto huku hasara kubwa katika miaka ya hivi karibuni sasa ikiwaacha nje ya kanuni za faida na uendelevu (PSR). ***(Football Insider)***

### SILVA AGOMBEWA EPL

ARSENAL, Manchester United na Liverpool zimefanya mawasiliano na Benfica kuhusu uwezekano wa kumnunua beki wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Antonio Silva, mwenye umri wa miaka 20.***(Caught Offside)***

### SLOT KUMSAJILI KOKCU

KOCHA mpya wa Liverpool, Arne Slot, amemweka kiungo wa kati wa Benfica na Uturuki, Orkun Kokcu, mwenye umri wa miaka 23, juu ya orodha yake ya wachezaji anaotaka kuwasajili ***(Givemesport)***

### RAYA KUBAKIA ARSENAL

ARSENAL itaanzisha kipengele cha chaguo lao la kumnunua mlinda lango wa Hispania, David Raya, mwenye umri wa miaka 28 na kufanya uhamisho wake wa mkopo kutoka Brentford kuwa wa kudumu msimu huu kwa pauni milioni 27. ***(Football Insider)***

### SPURS YAMYAKA CHALOBAH

KLABU ya Tottenham Hotspur imeiuliza Chelsea kuhusu kupatikana kwa Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24, wakati wakijiandaa kuanzisha ‚uvamizi' mara dufu kuipata sahihi ya beki wa Uingereza Conor Gallagher mwenye miaka 24. ***(HITC)***

## DO A SOKA MAGA ULAYA



# RASHFORD KUKOSA FAINALI EURO 2024

●●●Mshambuliaji huyo ameachwa katika kikosi cha England...

**LONDON, England**

KOCHA wa England, Gareth Southgate, alitaja kikosi chake cha muda cha wachezaji 33 kwa ajili ya mashindano ya Euro 2024 na kuwaita Eberechi Eze, Marc Guehi na Kobbie Mainoo huku Marcus Rashford au Jordan Henderson, hawakuitwa.

Southgate alijumuisha wachezaji watano ambao hawajawahi kuichezea England, Curtis Jones wa Liverpool na Jarell Quansah, Jarrad Branthwaite wa Everton, kiungo wa kati wa Crystal Palace, Adam Wharton na kipa wa Burnley, James Trafford.

Cole Palmer, Anthony Gordon na Ollie Watkins walitunzwa kwa misimu mizuri wakiwa na Chelsea, Newcastle na Aston Villa, huku fowadi wa Brentford, Ivan Toney, pia alijumuishwa licha ya kurejea Januari kutoka kufungiwa kwa miezi nane kwa kukiuka sheria za kamari.

Jack Grealish alichaguliwa licha ya kuanza mechi 10 pekee za Ligi Kuu England katika kampeni ya Manchester City ya kushinda taji, huku mwinuko wa Mainoo ukiendelea baada ya kucheza mechi yake ya kwanza ya ligi akiwa na Manchester United dhidi ya Everton iliyochezwa Novemba.

Mchezaji mwenzake na Mainoo, Luke Shaw amejumuishwa licha ya kuwa nje ya uwanja tangu Februari kutokana na jeraha la misuli.

Tarehe ya mwisho ya Uefa kuwasilisha kikosi cha mwisho ni Juni 7, mwaka huu wakati Southgate atalazimika kuchagua wachezaji 26 ili kwenda nao Ujerumani.

Namba iliyoongezwa ya Southgate iliyotangazwa kwenye Uwanja wa St. George's Park ni dalili ya aina mbalimbali za wasiwasi wa utimamu wa mwili ambao kocha huyo mwenye umri wa miaka 53 alikiri haukuwa wa kawaida katika kipindi cha miaka nane kama bosi wa England.

"Hatujawahi kuwa na hali nyingi zisizojulikana," alisema Southgate akiwaambua waandishi wa habari.

"Tumekuwa na mashindano ambapo tumechukua wachezaji ambapo tunajua watarejea kwa muda fulani wa mashindano.

"Kuna idadi kubwa, ambayo itaonekana kwako ukiangalia wachezaji ambao wamekosa michezo michache iliyopita ya msimu na wachezaji ambao wamerejea tu kwa michezo michache iliyopita ya msimu.

"Tuna changamoto muhimu ya kimwili kwa kuwa baadhi ya wachezaji watahitaji kazi zaidi, lakini lazima tuhakikishe tunasukuma kwa wakati sahihi, kupata dakika wanazohitaji katika michezo. Wachezaji wengine hawana.

"Kila mtu ana nafasi kwenye idadi ya watu 26. Hakika kuna baadhi ya wachezaji ambao tulitaka kuona. Sababu ya kikosi kirefu, tulikuwa katika hali kama hiyo kabla ya Euro zilizopita, na muda zaidi utatusaidia kufanya maamuzi bora na inaweza kutusaidia kutoa uwiano bora wa kikosi."

Gordon, nahodha, Harry Kane na Jarrod Bowen wa West Ham wote walikosa mechi zao za mwisho za klabu kutokana na jeraha huku James Maddison, Trent Alexander-Arnold na Guehi wamerejea hivi karibuni kutoka kwa kukosekana kwa muda mrefu.

Mshambuliaji wa Bayern Munich, Kane alikosa mechi mbili za mwisho za Bundesliga kwa timu yake kutokana na matatizo ambayo amekuwa akikabiliana nayo tangu kabla ya kupoteza mchezo wao wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Real Madrid wiki mbili zilizopita.

"Kane yuko wazi sana sasa," Southgate alisema. „Ametulia sana kuhusu hilo. Nadhani uamuzi wa busara ulichukuliwa kutosukuma mchezo wa mwisho huko.

"Matatizo ya mgongo yanaweza kutokea, lakini si jambo ambalo tunajali kwa wakati huu. Uelewa wetu juu yake ni jambo ambalo liko wazi sana sasa." Hata hivyo, Southgate alikiri matarajio ya Shaw kuthibitisha utimamu wake kwa wakati kwa Euro yalikuwa madogo.

## Kroos kustaafu baada ya Euro

**BERLIN, Ujerumani**

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Toni Kroos, atastaafu soka baada ya kuichezea Ujerumani katika michuano ya Euro msimu huu.

Kroos mwenye umri wa miaka 34, ameshinda mataji 22 akiwa na Madrid tangu alipojiunga mwaka 2014, yakiwamo mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na jingine akiwa na Bayern Munich na mataji manne ya LaLiga.

Kiungo huyo kwa mara ya kwanza aliibua matarajio ya kustaafu mwaka 2022, kabla ya kuamua kucheza kwa msimu mwingine, lakini sasa amechagua kumalizia soka lake msimu huu wa joto.

„Baada ya miaka 10, mwisho wa msimu sura hii inakamilika," aliandika Kroos katika ukurasa wake wa Instagram.

„Ningependa hasa kuwashukuru wote walionikaribisha kwa moyo wazi na kuniamini. Lakini hasa ningependa kuwashukuru, wapenzi wa Madrid kwa upendo wenu tangu siku ya kwanza hadi ya mwisho.

„Wakati huohuo uamuzi huu unamaanisha maisha yangu kama mwanasoka mwenye bidii yataisha msimu huu wa joto baada ya michuano ya Ulaya. Kama nilivyosema siku zote: Real Madrid ndiyo na itakuwa klabu yangu ya mwisho. Nina furaha na kujivunia, hilo akilini mwangu Nilipata muda mwafaka wa uamuzi wangu na ningeweza kuuchagua mwenyewe nia yangu ilikuwa ni kumaliza kazi yangu katika kilele cha kiwango changu cha utendakazi.

Kroos alitangaza kurejea katika soka ya kimataifa akiwa na Ujerumani Februari kabla ya michuano ya Euro, baada ya kustaafu soka ya kimataifa mwaka 2022.

Real Madrid ilishinda LaLiga msimu huu na itamenyana na Borussia Dortmund katika fainali ya Ligi ya Mabingwa huko Wembley Juni Mosi, mwaka huu.



# MAMA MBAPPÉ AFICHUA MWANAWE ANATUA MADRID




**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappé alipanga tafrija Jumatatu kuashiria kuaga kwake kutoka Paris Saint-Germain, ambapo mama ambaye ni wakala wake, Fayza Lamari, alidokeza atajiunga na Real Madrid msimu huu wa joto.

Takriban wageni 250 walihudhuria karamu huko Gigi, mgahawa wa hali ya juu wa Kitaliano karibu na Champs Élysées ya Paris.

Baada ya kuondoka ukumbini, Lamari aliulizwa ni wapi mtoto wake angecheza msimu ujao, na akajibu: „Nyote mnajua tayari."

Mbappé anatarajiwa sana kujiunga na Madrid akiwa tayari amethibitisha ataondoka PSG mkataba wake utakapokamilika msimu huu wa joto.

Vyanzo viliiambia ESPN anatarajiwa kujiunga na Madrid baada ya wababe hao wa Hispania kukabiliana na Dortmund katika fainali ya Ligi ya Mabingwa itakayochezwa Juni Mosi, mwaka huu.

## Alaba aachwa kikosi cha Euro

**VIENA, Austria**

NAHODHA wa Austria, David Alaba, ameachwa nje ya kikosi cha muda cha nchi hiyo cha Euro 2024, lakini beki huyo wa Real Madrid ambaye ni majeruhi ataandamana na kikosi kwenda Ujerumani kama 'nahodha asiyecheza,' Shirikisho la Soka la Austria, lilisema.

Kocha Mkuu wa Austrua, Ralf Rangnick, alitangaza kikosi cha wachezaji 29, akizingatia wimbi la majeraha ya hivi karibuni na ya muda mrefu.

Alaba, ambaye alicheza mechi mbili za awali za Austria za Euro 2016 na 2020, alipata jeraha kubwa la goti Desemba, mwaka jana.

„Ni aibu kubwa bila shaka hapatikani kwetu kama mchezaji. Wiki zilizopita nimekuwa na mazungumzo ya karibu na David. Alisisitiza alitaka sana bado kuwa nasi," Rangnick alisema.

„Kwa hiyo, nina furaha sana kusema hili litawezekana baada ya mazungumzo mazuri na klabu yake ya Real Madrid."



Kiungo, Xaver Schlager, atakosa michuano hiyo baada ya kujeruhiwa goti lake la kushoto mapema Mei, na pia kipa chaguo la kwanza, Alexander Schlager, ambaye alipata jeraha la goti.

Austria itamenyana na Ufaransa, Uholanzi na Poland katika Kundi D kwenye michuano ya Euro na itacheza mechi za kirafiki dhidi ya Serbia ifikapo Juni 4 na nyingine dhidi ya Uswizi hapo Juni 8, mwaka huu.

HABARI MICHEZO

# NBC YAANDAA SHEREHE ZA UBINGWA WA YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

WADHAMINI wakuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) imeandaa sherehe maalum kwa ajili ya kukabidhi kikombe cha ubingwa wa ligi hiyo kwa mshindi, Yanga itakayofanyika keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Yanga itakabidhiwa kombe la ubingwa baada ya kumalizika kwa mechi yao ya raundi ya 29 dhidi ya Tabora United.

Mkuu wa Idara ya Mahusiano na Mawasiliano wa NBC, Godwin Semunyu, alisema wao kama wadhamini wakuu wa ligi tatu tofauti hapa nchini wamejipanga kuhakikisha mabingwa wote wanakabidhiwa vikombe vyao kwa hadhi na heshima wanayostahili ikiwa ni ishara ya kutambua jitihada zao.

Semunyu alisema wanaipongeza Yanga kwa mafanikio licha ya ushindani mkubwa ulioshuhudiwa kwenye ligi hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa umechochewa na maboresho ya timu shiriki kufuatia udhamini wa benki hiyo.

"Ushindani huo unachochewa kwa kiasi kikubwa na udhamini wetu kama benki kwenye ligi hizi hatua ambayo imechangia kuviwezesha vilabu shiriki kufanya maandalizi mazuri bila changamoto za kifedha. Kwa kuzingatia mazingira hayo tumeona ipo haja pia ya kushiriki kikamilifu katika kuwapongeza washindi wote wanaopatikana kwenye ligi hizi...tunawapongeza sana," alisema Semunyu.

Naye Msemaji wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kupitia ushirikiano na benki hiyo wameandaa tukio kubwa la kusherehekea ubingwa litakolihusisha matukio mbalimbali ikiwamo mkesha wa sherehe na 'parade' itakayoanzia uwanjani hadi makao makuu ya klabu hiyo.

Kamwe alisema watalitembeza kombe lao la ubingwa kwa kutumia helikopta 'Chopper' maalum itakayozunguka maeneo mbalimbali ya jijini ili kunogesha shughuli hiyo.

"NBC wametuheshimisha sana katika sherehe hizi wakiwa kama wadhamini wakuu wa ligi hii. Mbali na kutusaidia kufanya maandalizi ya sherehe hizi za ubingwa pia wamejipanga kuhakikisha wanasajili wanachama wetu pale uwanjani na kuwapatia kadi za uanachama za kisasa hatua ambayo ni muhimu sana hususani katika kutuongezea mapato ya klabu. Tuwashukuru sana na tunawaomba wanachama na mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi siku ya tukio hilo muhimu," Kamwe alisema.




Msemaji wa Yanga, Ali Kamwe (kushoto), akizungumzia maandalizi ya sherehe ya kukabidhiwa kombe la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kutoka kwa mdhamini mkuu wa ligi hiyo, Benki ya NBC. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Mahusiano ya Umma na Mawasiliano wa NBC, Godwin Semunyu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgunda amkubali Chasambi

**Na Faustine Feliciane**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema uwezo ulioonyeshwa na mchezaji wake, Ladack Chasambi, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold uliochezwa ni wa hali ya juu na kumtaka nyota huyo kuendeleza makali yake ili afike mbali.

Katika mechi hiyo Simba iliibuka na ushindi wa mabao 4-1 huku Chasambi akifunga magoli mawili.

Matokeo hayo yameifanya Simba kufikisha pointi 63 sawa na Azam FC iliyoko katika nafasi ya pili, ikipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya JKT Tanzania, mechi ikichezwa mapema juzi.

Mgunda alisema kama mchezaji huyo ataendelea kujituma na kudumisha nidhamu anaamini atafika mbali kutokana na uwezo wake na kipaji alichonacho.

„Kila mchezaji amepambana kwa ajili ya timu, tumetoka nyuma na kupata ushindi, nawashukuru wachezaji lakini pia nimsifie Chasambi kwa namna alivyojituma, ni mchezaji mdogo lakini mwepesi kushika na kuyafanyia kazi maelekezo ya mwalimu," alisema Mgunda.

Kocha huyo aliongeza mechi mbili zilizobakia ni kama fainali kwao kwa sababu wanahitaji ushindi ili kujaribu kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Tayari Yanga imeshatangazwa mabingwa na vita iliyobakia ni ya kumaliza katika nafasi ya pili ili kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Gamondi: Soka la Bongo limekua

INATOKA UK. 24

mkubwa, kuna utofauti mkubwa kati ya timu tatu za juu na zinazofuata chini ya msimamo, labda ni suala la bajeti, lakini natamani misimu ijayo kuwe na mabadiliko ushindani kutoka katika klabu nyingine, kuwe na uwiano wa ushindani na si hivi," alisema kocha huyo.

Raia huyo wa Argentina pia alionekana kukerwa na baadhi ya viwanja nchini kuwa vinawakwaza makocha wanaofundisha timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Viwanja bado vina changamoto, navyo vifanyiwe kazi, kukiwa na viwanja vizuri kunatoa nafasi kwa wachezaji kucheza vizuri na makocha kufanya kazi kwa uhakika zaidi ikiwamo kupata mafanikio.

Nashauri pia makocha wazawa wapewe elimu ya kuwa makocha wazuri, wapewe nafasi na waaminike kufanya kazi, vile vile kuna tatizo katika utengenezaji wa vipaji vipya katika soka la vijana, bado nguvu iongezeke.

Wachezaji wa kigeni waliopo wamelifanya soka la Tanzania kufahamika na kuheshimika zaidi, lakini wanafanya kazi kubwa na kuwa chachu ya wazawa kujituma katika vikosi ili kupigania namba, pia hata wachezaji vijana kujifunza kutoka kwao.

Aliongeza wachezaji hao wageni waendelee kuruhusiwa kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sababu uwepo wao ‚umenogesha' ligi na kuipa heshima katika ubora wa viwango vya soka Afrika.

Gamondi ataiongoza Yanga katika sherehe za kukabidhiwa kombe la ubingwa Jumamosi baada ya mechi dhidi ya Tabora United itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Fei Toto: Tunaitaka Ligi ya Mabingwa

INATOKA UK. 24

toke kwenye mbio zetu za kumaliza katika nafasi ya pili," alisema kiungo huyo.

Aliongeza michezo yote iliyobakia ni ya presha kwa sababu pia Simba wanaihitaji nafasi hiyo ili kujihakikishia tiketi ya kushiriki katika michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

"Hatutaki kuangalia michezo yao au matokeo yao (Simba), kikubwa sisi ni lazima tufanye vizuri katika michezo yetu, kuteleza kwa namna yoyote kutatuondoa kwenye nafasi hii, tutakuwa makini mpaka mwisho wa msimu," alisema Fei Toto.

Wakati huo huo, Fei Toto ameendelea kujiimarisha katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu baada ya kufikia mabao 16, moja zaidi ya mshambuliaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki.

"Nashukuru nimefunga na kuisaidia timu yangu kupata ushindi, kwangu mimi kitu kikubwa ni matokeo ya timu, kumaliza nafasi ya pili, kama itatokea nimepata tuzo ya ufungaji bora ni sawa, nitafurahi lakini kikubwa kwa sasa nafunga si kwa ajili ya kiatu cha dhahabu, bali kwa ajili ya timu kupata matokeo mazuri ili kama timu tufikie malengo yetu ya sasa," alisema Mzanzibari huyo.

Yanga itafunga pazia la msimu huu kwa kuwakaribisha Maafande wa Tanzania Prisons kutoka jijini, Mbeya.

Michezo
Alhamisi Mei 23, 2024
Nipashe

## Rashford kukosa Fainali Euro 2024

UKURASA 21







# Gamondi: Soka la Bongo limekua

●●● Hata hivyo akerwa vigogo kutawala, rasmi Fainali FA kuchezwa Zanzibar...

Beki wa kushoto wa Yanga, Joyce Lomalisa (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Dodoma Jiji FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma jana. Yanga ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Shirikisho la Soka Nchini (TFF), limetangaza rasmi kupeleka Fainali ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema soka la Tanzania limekua ingawa baadhi ya mambo yanatakiwa kufanyiwa maboresho.

"Uamuzi huo umefanywa na Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania baada ya baadhi ya miundombinu muhimu mjini Babati kutokuwa tayari kwa ajili ya fainali hiyo pamoja na sababu za kiusalama.

TFF, imezishauri mamlaka za mikoani Manyara kuendelea kufanya marekebisho katika miundombinu hiyo ili ifikiriwe kwa ajili ya fainali zijazo na michuano mingine mikubwa," ilisema taarifa iliyotolewa na TFF.

Taarifa hiyo iliongeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, atakuwa mgeni rasmi katika fainali hiyo itakayowakutanisha Yanga dhidi ya Azam Juni 2, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili, Gamondi akiwa na msimu mmoja tu nchini amesema ili Ligi Kuu Tanzania Bara iwe bora zaidi ushindani kutoka katika timu nyingine unatakiwa kuongezeka na kuacha utawala wa timu tatu za Simba, Yanga na Azam.

Gamondi alisema kama hali itabakia hivi ilivyo, vigogo hao watatu watakosa ushindani na badala yake wataendelea kutawala kwa muda mrefu soka la Tanzania.

Alisema pia ili kufanya vizuri kwa timu ambazo zinafundishwa na makocha wazawa, inahitajika walimu hao wazalendo kupatiwa elimu huku nguvu ikiongezwa katika maendeleo ya soka la vijana.

Kocha huyo pia amewapongeza wachezaji wa kigeni kwa kusaidia 'kulichangamsha' soka la Kibongo pamoja na nyota wake kwa ujumla ambao wameonekana kujifunza kutoka kwa wenzao.

"Nchi imepiga hatua kubwa kwa ujumla kwenye soka, lakini bado natatizwa na ushindani kwenye ligi, kwa sababu ni timu tatu tu ndizo zenye ushindani na zenye uwezo

INAENDELEA UK. 23

## Fei Toto: Tunaitaka Ligi ya Mabingwa

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya JKT Tanzania, kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Feitoto' amesema wanapambana katika michezo iliyobakia kwa sababu nia na malengo yao ni kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Azam FC yenye pointi 63 sawa na Simba iko katika nafasi ya pili, ikiwa na idadi nzuri ya mabao ya kufunga ukilinganisha na Wekundu wa Msimbazi wakati Yanga tayari imeshatwaa ubingwa.

Fei Toto aliliambia gazeti hili wachezaji wa Azam FC hawataki kuona wanapoteza mechi yoyote katika michezo miwili iliyobakia ili kufikia ndoto za kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika zitimie.

"Tunashukuru tumepata ushindi katika mchezo wetu dhidi ya JKT, ulikuwa mchezo mgumu lakini ilikuwa lazima tupate ushindi ili tusi-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >